

BWANA YESU ALIYEFUFUKA



Habari za jioni marafiki. Tuna furaha kuwa Phoenix usiku wa leo kwenye ibada hii, lakini tunasikitika kuwa ndio usiku wa mwisho. Na kwa hiyo tunatumaini kwamba Mungu atatupa baraka Zake kuu usiku wa leo, kwamba hakutakuwako na mgonjwa miongoni mwetu tutakapoondoka usiku wa leo, pasipo na mtu anayeteseka. Ninawatakeni hapa, kwenye machela, vitanda, na viti, nataka mnifanyie jambo fulani usiku wa leo. Nataka uamini kwa moyo wako wote. Ningependa kuona kila mmoja wenu akitoka usiku wa leo, mzima.

² Anawapenda, enyi marafiki. Kwa sababu tu magonjwa na mambo yenu yanaonekana kuwa hayatibiki, huyo ni Shetani tu anayewaambia hivyo. Si zaidi Kwake kukuponya, kuliko kumponya mtu yeyote. Wewe amini kwa moyo wako wote usiku wa leo. Amini tu; haileti tofauti yoyote jinsi wewe. . .yale akili yako inasema juu yake; chukua tu kile Mungu anachosema juu yake. Najua ni kweli. Nisingekwambia hilo, kama nisingalijua kweli kwamba hiyo ilikuwa ni kweli kabisa.

³ Sasa, tunataka kushukuru, kwanza...Nadhani, Ndugu Moore, kwa kawaida meneja hufanya hivi, lakini na—nataka kuchukua fursa hii, mimi mwenyewe, kushukuru kila mmoja wenu kwa kusaidia kufanya mkutano huu kuwa bora zaidi, ninaamini, ambao umefanya...tume kuwa nao Phoenix; wa kiroho zaidi na uliotulia kuliko mkutano wowote ambao nimekuwa nao Phoenix.

⁴ Ninataka kushukuru kundi hili zuri la wahudumu, wahudumu wanaoshirikiana, ambao walitusaidia kuwa na mkutano huu, wafadhili wote. Wengi wao hawangeweza kufadhili, maana walikuwa na miamsho yao wenyewe na mambo yakiendelea. Hatujaribu kamwe, loo, kufanya jambo kubwa sana, kuninii, ati kila mtu hana budi kufunga makanisa yao. Baadhi ya ndugu walikuwa na mahema makubwa na kadhalika; hawana budi kuwa nayo...kila mtu hana budi kufunga la sivyo hawawezi kuja. Vema, sijawahi kufanya mkutano wangu namna hiyo tu. Ninaifanya rahisi na midogo, na ili kwenda tu na kufanya vema niwezavyo.

⁵ Nawashukuru wote waliokuja, na wale ambao hawakuweza kuja, mbona, ninawashukuru vivyo hivyo. Nayo matumizi yetu kwa njia hiyo yako chini, bajeti yetu si kubwa sana kutengeneza; na kwa hiyo basi, haitupasi kuwasumbua watu, tunachukua tu toleo la kawaida na kuyalipia madeni yetu. Mara tu bajeti inapotengenezwa, hilo latosha.

⁶ Na ninasikia kwamba usiku wa leo wamenitolea sadaka ya upendo; hakika nathamini hilo. Laiti haikunibidi, kuichukua.

Lakini nina wajibu mkubwa tu; mnaweza kuwazia kile ulicho. Na ofisi ikiendelea wakati wote; wajibu wangu ni kama dola mia moja kwa siku, haidhuru niko wapi. . . Hiyo ni Jeffersonville pekee, haidhuru kama niko kwenye ibada ama siko. Mnaweza kutambua jinsi ninavyorudi mbali shimoni, wakati mwingine.

⁷ Na sasa, tunatuma vitambaa vingi sana vya maombi, kama hivi *hapa*. Nasi tunavituma kote duniani. Wakati mwingine kama elfu moja kwa siku, tumevituma. Nanyi nyote mumekaribishwa, wakati wowote ambapo ninaweza kuwa msaada kwenu, mbona, niandikieni na kunijulisha. Sisemi kwamba. . . Mnaona, mara nyingi wanasema, “Niandikieni,” ili tu kupata anwani yako. Lakini sina vipindi vyovyote vya redio vya kufadhili. Sina chochote, ninii tu. . . wewe. . . Hakuna kitu ambacho. . . mimi, ili tu niweze kuwasaidia. Kuwatumia tu kitambaa cha maombi ama kitu kingine, ningefurahi kufanya hivyo. Nikuombe, nitafurahi kufanya hivyo.

⁸ Na sasa, ninataka kushukuru kila mmoja wenu kwa ushirikiano wenu. Ninyi nyote watu ambao mumekuwa mkija, yote mliyotoa, na sadaka ya upendo usiku wa leo, kila senti ambayo si lazima iende kwenye maskini ninii yetu. . . Maisha tuliyo nayo, tunaishi maskini kama tu watu wengine. Watu hawawezi kuelewa hilo: kwa nini nimekuwa hudumani muda mrefu kuliko wengine wote, na hata hivyo sina chochote. Ni kwa sababu mimi hutumia kidogo nilicho nacho katika misheni za nchi za kigeni, rafiki, kila kitu. Mungu ndiye Hakimu wangu mkuu wa jambo hilo, mnaona, ya kwamba kila kitu ninachopata, mimi. . .

⁹ Kama. . . Katika mambo ya kifedha, kama tukijaribu kuishi kawaida, kama watu, halafu kile kidogo tulichobakiza, nakiongezea, nakiongezea, mpaka nipate cha kutufikisha kwenye nchi za ng'ambo. Tunaenda huko na kuhubiri Injili, basi, kwa wale ambao hawakuwahi kuisikia hapo awali, na kuwaleta maelfu mara maelfu na maelfu kwa Kristo. Pesa zetu zinapoisha, tunarudi, tunakuja Marekani, na kuwapitia na kuwatembelea marafiki zetu. Wanatusaidia kidogo, na mara tu tunapopata akiba ya kutosha, tunaondoka tena.

¹⁰ Sasa, najua hilo, nina marafiki wengi. Ninao marafiki walioketi moja kwa moja katika jengo hili, usiku wa leo, wangesema tu, “Haya Ndugu Branham, nitakuandikia hundi uende kwenye nchi za ng'ambo.” Lakini hiyo haingekuwa sawa kwa watu wengine. Mnaona? Kila mmoja wetu anataka sehemu ndogo katika hilo. Hiyo ni kweli. Kila jamaa na senti zake, senti kumi na tano, robo, chochote kile, hiyo ni sehemu katika Ufalme. Na kwa njia hiyo, basi ninajua ni Bwana akinituma kule.

¹¹ Nadhani kabla sijawaona tena, labda nitakuwa na ziara nyingine ya nchi za ng'ambo. Moja inakuja sasa kwa ajili ya Afrika nzima; Tanganyika, Rhodesia, kote hata kuingia

India tena. Na kwa hiyo, tunatumaini ya kwamba mtakuwa mkituombea, tunapoendelea.

¹² Nilikutana na rafiki mmoja leo, akaniambia nisitaje jina lao kutoka jukwaani, lakini kwamba wapo, wanajua jinsi tunavyowathamini, kila mmoja wao. Ninawapenda kwa moyo wangu wote. Halafu basi, baadhi ya watu wamekuwa... Wanajua kuwa mimi ni... napenda kuwinda vizuri sana, kwa hivyo nimelishwa vizuri kwa wanyama pori. Waliniletea... watu wawili au watatu walileta paa mahali nilipokuwa nikiishi; wakaleta kulungu, na hata nyati, na nguruwe mwitu, hivyo mimi ni—nilikuwa na wakati mzuri tu.

¹³ Hiyo ni mara yangu ya kwanza kwa baadhi ya hizo. Zilikuwa nzuri sana. Bwana awabariki. Laiti mngalijua jinsi nilivyozipenda hizo. Nami nawashukuru sana. Na mara ya kwanza niliwahi kuonja nguruwe mwitu ama—ama nyati, na ilikuwa tamu kweli. Nami ninashukuru sana. Na kulungu na paa walikuwa watamu sana. Nami ninapenda sana vitu vya aina hiyo. Sijui ni kitu gani kinanifanya nivipende, lakini mimi—mimi navipenda kwa vyovyote vile. Ninapenda misitu na porini, kwa hivyo napenda kile kinachoambatana nayo. Kwa hivyo nawashukuru sana, sana.

¹⁴ Na sasa, kwenu nyote mliokusanyika huku, imani ya ajabu, mumekuwa wazuri sana. Mkutano umekuwa mgumu kidogo kwangu, marafiki. Hii imekuwa mara ya kwanza katika mikutano yangu ambapo nimewahi kujaribu kufanya wito wangu mwenyewe wa madhabahuni; kuhubiri, kufanya wito wangu wa madhabahuni, kuwaleta watu kwa Kristo, kisha kuwaombea wagonjwa; imekuwa ngumu sana. Kwa siku chache zilizopita, karibu nibwagwe nje. Maana huu sio mkutano pekee ninaohudhuria.

¹⁵ Ninaelekea moja kwa moja huko California. Tumepakia mara moja, karibu mizigo yetu yote, tayari kuondoka kuelekea California. Nasi tutakuwa kule, kisha turudi moja kwa moja, Macon, Georgia. Moja kwa moja kutoka huko hadi Colorado, na kuendelea zaidi na zaidi, na bila shaka kidogo inachosha.

¹⁶ Jinsi wakati mmoja... Furaha kuu zaidi ambayo nimekuwa nikipata katika mikutano yangu, haswa hivi karibuni... Sikuzote namwachia meneja ama mtu fulani wito wa madhabahuni. Lakini mimi... Inanipa msisimko ulioje kuona watu wakisimama na kumkubali Bwana Yesu kama Mwokozi wao binafsi. Nami ninafurahia hilo sana.

¹⁷ Nami nataka kufanya... Nataka wahudumu waelewe hili, kwamba, wafadhili wangu na wale walio karibu, ningependa kurudi Phoenix wakati mwingine, Mungu akipenda, kufanya tu mkutano wa kuhubiri Injili tu, na kuwaleta watu madhabahuni, na kuwawekea mikono ili wampokee Roho Mtakatifu. Kwa upambanuzi huu, maono ndiyo yanayoniwaga chini hivyo.

¹⁸ Je, mngependaje turudi na kufanya mkutano kama huo? Je, mngependa kufanya hivyo? [Kusanyiko linashangilia—Mh.] Vema, Mungu awabariki. Asanteni sana. Labda niwaombee wagonjwa, lakini si chini ya upambanuzi, ili niweze kukaa muda mrefu, mnaona; badala ya kukaa tu siku chache usiku kisha inibidi kuondoka, mbona, tungeweza kukaa muda mrefu zaidi. Asanteni sana.

¹⁹ Ninapofanya ziara yangu nchini kote sasa, kabla ya kwenda kwenye nchi za ng'ambo, ninauliza hilo. Na huko Los Angeles kwa Wafanyabiashara Wakristo, siku tano za kwanza usiku ni kuhubiri tu, na kuweka mikono juu ya wagonjwa, na kuwaombea wanapopitia mstarini. Tunamshika kila mtu basi.

²⁰ Na sasa, hivyo sivyo hasa jinsi ninavyotumia huduma yangu, bali ni jinsi watu wanavyofundishwa, nao wanaamini kwa ajili hiyo, kwa hiyo ningependa kufanya hivyo kwa muda. Kamwe huwezi kulichanganya, maana maono yanapoanza basi huna uwezo wa kuyadhibiti; yanaendelea tu kutokea. Na sasa, laiti, usiku wa leo, ningaliweza kuwaelezea na kuwaambia jinsi hilo hutukia, bali siwezi. Hilo ni fumbo kubwa sana kwangu kama lilivyo kwenu.

²¹ Sasa, nafikiri ya kwamba hilo linajumlisha kila kitu, isipokuwa walinzi, na mabawabu, na kadhalika. Tunashukuru udugu huu wa Shriner kwa kuturuhusu kutumia ukumbi huu. Natumaini kwamba walinzi, na wasimamizi, na kadhalika wapo. Ikiwa hawapo, naomba muwape shukrani nyingi mno. Hii ni mara ya pili wameturuhusu kuutumia, nasi tunashukuru kwa ajili ya hilo. Bwana awabariki wote.

²² Na mabawabu ambao wamekuwa wema sana kutusaidia kuandaa mstari wa maombi; na hasa sana maskini bawabu mmoja ambaye amekuwa akija pamoja na Billy, akinisaidia, hapa nje; jamaa mdogo, maskini jamaa mzuri sana, niliweza kumpa mkono muda mfupi uliopita. Na wakati wanaponileta humu ndani, hawazungumzi, kwa vile mtu yeyote anajua hivyo, kwa hivyo tunafika jukwaani baada ya kutoka kwenye maombi.

²³ Na hakika tunamshukuru huyo ndugu. Na hao wengine, pia, Ndugu Ballard na kundi hili zuri la ndugu wanaoketi hapa nyuma, Ndugu Falk, ama, Fuller, na loo, wengi sana. Ninajua sura zao lakini wakati mwingine siwezi kukumbuka jina lao. Nadhani ni watu wazuri sana. Nami naamini mmoja wao, ninaamini ni Ndugu Fuller, anaanzisha uamsho mara baada ya huu, sivyo? Naam, kesho usiku, tuna hakika, nitafanya tangazo hilo, kwamba Ndugu Fuller hapa, wa (Je, ni Maskani ya Fuller? Ndivyo mnavoyoiita?) Maskani ya Imani. Je, tayari mumelitangaza hapa? Nadhani hata hivyo. . .

²⁴ Nasi tunafurahi tu kutangaza uamsho wowote, wakati wowote, na, ama, mahali watakapokuwa. . .Hima, upesi, kila mtu ahudhurie uamsho huu unaotangazwa sasa, na uendele

moja kwa moja na kumtumikia Bwana. Usiache taa yaa nyumba yako izime. Endelea tu kuhudhuria miamsho hii.

²⁵ Loo, ni ajabu sana kujua kwamba Bwana Yesu yu hai leo, sivyo? Anaishi na kutawala mioyoni mwetu. Na sasa usiku wa leo sitaki kuchukua muda mwingi sana. Ninataka kunena kwa muda kidogo tu juu ya Neno, kisha niende moja kwa moja kwenye mstari wa kuwaombea wagonjwa.

²⁶ Kidogo niliwaambia kutangaza kwa namna fulani, kwamba labda ningepiga simu tu. Na basi kwa namna fulani ninajisikia kama, labda, tumwachie tu Bwana, tuone atafanya nini juu yake, kwamba, hadi mwisho wa—wa safari, tutakapoufikia wakati huo. Wakati mwingine Yeye hutuacha tu tuende moja kwa moja hadi dakika ya mwisho, ndipo atwambie la kufanya. Kwa hiyo tunampenda kwa ajili ya hilo, sivyo?

²⁷ Sasa, Bwana awabariki. Nanyi mniombee. Ni wangapi wataniahidi kuwa wataniombea? Mimi—mimi tu... Mungu awabariki, loo, jamani, watoto. Na—nawazia tu kuingia na kupeana mikono na watu. Na jinsi ningependa tu kushuka kupitia kwenye marefu haya ya kanisa usiku wa leo. Mimi... ukweli kabisa, ningependa kwenda nyumbani na kila mmoja wenu, tuketi usiku kucha, tuketi na kuzungumza kwa muda, tuamke asubuhi na kuzungumza. Jinsi ningependa kufanya hivyo; moyo wangu unatamani sana kukutana na watu hivyo. Lakini karibu inanilazimu kuwa mtu wa kujitenga kwa sababu ya aina ya huduma niliyo nayo, maana ni, siwezi kabisa kufanya hivyo na kufanya mkutano. Lakini Mungu anajua kwamba ninawapenda.

²⁸ Kwa hiyo ninaweka miadi na kila mmoja wenu, ya hii, nitakapowaona katika ile Nchi Tukufu, kama Mungu akiniruhusu kuwa kule pamoja nanyi, ninataka tu kwenda huku na kuketi miaka elfu moja pamoja na kila mmoja wenu na kuzungumza. Nasi tuta—tutaninii tu, hatutakuwa na muda mfupi wa kuzungumza kuliko tulipoanza. Tutazungumzia yote basi, sivyo? Hilo si litakuwa zuri sana, kuketi chini ya Mti wa Uzima?

²⁹ Nanyi mnajua, tutatumbuizwa na... waimbaji wote mashuhuri. Kutakuwako na Sankey, na Beverly Shea, na hao wote, kule kilimani kule, wakiimba tu sifa za Mungu. Tutakuwa tukiketi kando ya Mti wa Uzima, ambapo maji yanatoka chini ya kile kiti cha enzi. Je, hilo si litakuwa la ajabu? Naitamani tu siku hiyo. Inajalisha nini kwa Mkristo ambaye kweli ametia nanga ndani ya Kristo? Kwa maana mara tu maskani hii ya kale iliyo ya dunia hii ikiondolewa, tunaingia moja kwa moja ndani ya nyingine, moja kwa moja huko juu. Jamani, si ni ajabu hilo?

³⁰ Wazia: wagonjwa, na wachovu, na waliovurugika, na wenye huzuni ya moyo, kila kitu kikienda vibaya, ulimwengu wote

umejaa machafuko, wewe unawazia, “Vema, njoo, Bwana Yesu.” Muda si muda mwajua, mwili huu wa kale unaotetemeka unaanza kunyauka, nawe unahisi maumivu yakipitia ndani yake, mauti baridi yakinyemelea kifichifichi. Ndipo unaangalia ukisimama kule: kule kuna mwili mpya kabisa, umesimama huko ng’ambo; unaondoka tu kutoka kwenye huu, unaingia moja kwa moja katika ule.

³¹ “Maana maskani hii iliyo ya dunia ikiharibika, tunayo moja inayongoja tayari,” kuhamia humo. Mpya, usiofanywa kwa mikono, bali Mungu ndiye aliyeufanya, umeumbwa Milele, utukufu wa Mungu; kuhamia moja kwa moja humo, kufanyika mpya na mchanga tena, kutokuwa mgonjwa tena. Loo, jamani, nini kinaweza. . . Mbona mauti hayana m—mshiko wowote kwa Mkristo, sivyo? Mauti ni kitu tu cha kumleta Mkristo moja kwa moja katika Uwepo wa Muumba wake. Yeye ni mzuri sana unapoweza kumwazia hivyo, sivyo? Jinsi mauti hayawezi kumshika Mkristo, yanampeleka tu moja kwa moja. . .

³² Sasa, kwamba huo utakuwa mwili wa aina gani, kabla hatujarudi kuuchukua mwili huu, sijui; haijafunuliwa kwa mwanadamu bado. Lakini tunajua kwamba hatutakuwa roho baada ya kuondoka hapa. Roho itaiacha maskani hii, kuhamia ile ambayo Mungu ameifanya. Sio roho tu; ni mwili. Amina. Una umbo, mtindo, kila kitu. Loo, hiyo itakuwa ni ajabu sana, sivyo?

³³ Sasa, kusoma kidogo tu kutoka katika Neno, maana Maneno Yake hayatashindwa; maneno yangu yatashindwa, na neno la mtu mwingine yeyote litashindwa, lakini Neno Lake halitashindwa. Kwa hivyo katika Luka Mtakatifu. . . Nimekuwa nikihubiri sana kuhusu Agano la Kale, nilifikiria, usiku wa leo, ningebadilisha kidogo, na kupata kutoka kwenye li—lile Jipya. Mimi nikiuwa tu ni mfananishaji, kidogo inanibidi kurudi nyuma na kuchukua mstari wa Agano la Kale, nipate kujua jinsi lile Jipya linavyoonekana. Kwa hivyo naamini kama ningekuwa na kivuli cha kitu hicho, nitajua takriban kilivyo kinapofika hapa, kama tukiona kivuli chake.

³⁴ Sasa, katika Agano Jipya, Luka Mtakatifu m—mlango wa 24, na kuanzia kifungu cha 30. Kwa njia tu ya somo, tunasoma hivi, kif- . . . vifungu hivi.

Ikawa alipokuwa ameketi nao chakulani, kwamba alitwaa mkate, akaubariki, akaumega, akawapa.

Yakafumbuliwa macho yao, wakamtambua; kisha akatoweka mbele yao.

Wakaambiana, Je, mioyo yetu haikuwaka ndani yetu, hapo alipokuwa akisema nasi njiani, na kutufunulia maandiko?

³⁵ Sasa, hebu na tumwombe, Bwana Yesu aliyefufuka, kama hatatufungulia Maandiko sasa, wakati tunapoketi na kumngoja Yeye. Twaweza kuinamisha vichwa vyetu, tunapomba?

³⁶ Mwokozi wetu mpendwa, tumekuja Kwako usiku wa leo, kwa mioyo iliyo wazi, kama tunaijua. Tunakuja Kwako na hakikisho hili lililobarikiwa, ambalo limewekwa katika utu wetu wa ndani kabisa, ya kwamba Wewe ndiwe Mwana wa Mungu aliye hai, kwamba ulikufa kwa ajili ya dhambi zetu, na kututenga, basi, na dhambi, na umefufuka katika wafu, na sasa umeketi mkono wa kuume wa Ukuu huko juu, na umemtuma Roho Mtakatifu kurudi.

³⁷ Nasi tunakushukuru kwa ajili ya ushuhuda wa Roho Mtakatifu, akithibitisha Maneno kwa ishara inayofuata. Tunakushukuru kwa ajili ya mkutano huu mkuu, wa ajabu, ambao ni kwa neema Yako tu tumeweza ku—kushiriki. Jinsi tumeshiriki kwenye Neno, na kwa Roho wa Mungu. Sisi sote, tukiwa ni wa madhehebu mbalimbali, tuseme, bali sote pamoja, na tumeketi katika mahali pa Mbinguni katika Kristo Yesu, ameifungua mioyo yetu kwa Neno na kumwacha Roho Mtakatifu apate kuingia. Utulishe.

³⁸ Mamia wamekupokea Wewe kama Mwokozi wao; tunashukuru sana kwa ajili yake. Na wagonjwa, vilema, wale ambao wamekuwa wakiketi kwenye viti vya magurudumu, waliopooza, waliolala kwenye vitanda, machela, wameponywa na wakatoka nje. Vipofu, viziwi, bubu, magonjwa ya kila namna yameponywa. Na Wewe, Ee Mungu, umekuja katikati ya watu, nayo imani yao imevutia maneno ya kimbinguni, yakiwaelezea maisha yao, yale wamefanya, na yale wanayopaswa kufanya, na yale yatakuwakuwapo.

³⁹ Mungu, tunashukuru sana kujua kwamba Yesu yu hai leo. Nasi tunaomba, sasa, ya kwamba atakuja na kuchukua ibada na kuishughulikia Mwenyewe. Mtakase kila mtu aliye humu ndani katika kulisikia Neno usiku wa leo. Utusamehe kupungukiwa kwetu kwote. Nisaidie usiku wa leo, Baba. Nena Neno katika kuwaombea wagonjwa. Na ibada itakapomalizika, na tuseme kama wale waliotoka Emau, “Je, mioyo yetu haikuwaka ndani yetu, kwa sababu ya Uwepo Wake?” Kwa maana tunaomba katika Jina Lake. Amina.

⁴⁰ Somo letu usiku wa leo, ni, *Bwana Yesu Aliyefufuka*. Kidogo ni mada ya msingi kwa ajili ya uamsho wetu. Mada ya uamsho wetu imewekewa msingi kwenye Waebrania 13:8, kwamba, “Yesu Kristo ni yeye yule jana, leo na hata milele.” Kwamba Yeye ni yeye yule katika kanuni, ni yeye yule katika upendo, ni yule yule katika uwezo, yeye yule hasa kabisa; Yeye ni yule yule katika Kanisa Lake. Sasa, Yeye hayuko hapa katika umbo la mwili. Yeye yuko hapa katika umbo la Roho nao mwili Wake ulitwaliwa juu.

⁴¹ Tunaamini kwamba Mungu alifanya agano na jamii ya wanadamu pale Kalvari. Nalo lilifanywa chini ya haki za njia za Mashariki za kufanya agano. Chini ya njia ya Kimashariki

ya kufanya agano, walimchinja mnyama, wakampasua, wakaandika agano, wakalipasua vipande viwili juu ya huyo mnyama aliyekufa, mtu mmoja akachukua sehemu moja, na mmoja, hiyo nyingine. Wakati vitakapokutana, vipande hivyo lazima viumane pamoja la sivyoyaitabidi kulitimiza hilo agano. Kwa hiyo wakala kiapo, ya kwamba, miili yao na iwe kama huyo mnyama aliyekufa kama wakikosa kulitimiza hilo agano.

⁴² Hivyo ndivyo Mungu alivyofanya pale Kalvari. Aliuchukua ule mwili na mahali alipokaa, Kristo Yesu, ukapasuliwa na kukatwa vipande. Mwili ukatwaliwa kwenye mkono wa kuume wa Ukuu huko juu na Roho Mtakatifu akaletwa hapa duniani. Na sasa, Roho yeye yule aliyekuwa ndani ya mwili huo anaishi katika Mwili wa Mkristo usiku wa leo. Na katika ufufuo, mwili uo huo itabidi upatane, kisha uje pamoja, Roho yeye yule aliyekuwa ndani ya Kristo Yesu hana budi kuwa ndani yako la sivyoyhutafufuka. Je, mnaweza kuliona?

⁴³ Tazama jinsi Mungu, hapo mwanzo, huko nyuma kabisa, alivyofunika anga lote na wakati, na kutoka kwa Mungu akatokea Logos aliyetoka kwa Mungu, ambaye alikuwa ni sehemu ya Mungu. Mungu akiona vile mwisho ungekuwa, tangu mwanzo, naye Logos akaja duniani, ambaye alikuwa ni Kristo Neno, Neno lililonenwa la Mungu, sehemu ya Mungu, naye akafanyika mwili akakaa miongoni mwetu. Halafu basi, sisi tulitoka kwa Kristo, ambalo linaufanya Uzima ule ule uliokuwa ndani ya Mungu, katika Kristo, kuwa ndani yako. Na kwa hakika tu kama vile Mungu alivyomfufua Huyu, hatuna budi kuja na jambo lile lile, ikiwa Roho yuyo huyo yuko ndani yetu, kwa sababu ni Roho wa Mungu akitufanya wana na binti za Mungu.

⁴⁴ Loo hiyo si ni ajabu? Je, tunampataje? Kwa kumwamini Bwana Yesu Kristo, ndivyo hivyo. Kumkubali, na kisha Mungu kwa kuitikia, hutupa Roho Mtakatifu, tukilia mioyoni mwetu, “Aba Baba, Mungu wangu, Mungu wangu.” Na kisha tunafufuliwa katika siku za mwisho tupate kunyakuliwa. Naye alisema, “Siku hiyo mtajua ya kuwa Mimi ni ndani ya Baba, na Baba ndani Yangu, Mimi ndani yenu, nanyi ndani Yangu.”

⁴⁵ Huyu hapo Roho akitoka kwa Mungu, akidhihirishwa kama Logos, akashuka na kufanyika mwili, akakaa miongoni mwetu, ambapo alifu...alikuwa, akachukua adhabu ya dhambi, akafufuka tena, akiketi kwenye Ukuu juu, kwenye mkono wa kuume wa Mungu. Naye Roho Mtakatifu akirudi, akileta Roho yeye yule ndani ya watu binafsi sasa, ili kuwarudisha katika uhusiano na Muumba wao. Je, si ni ajabu hivyo?

⁴⁶ Hivyo basi mabomu yote ya atomiki, na ninii yote. . . Mliona lile gazeti leo? Inaonekana kana kwamba vita vinakaribia kuvuma tena; wanaipindua bunduki yao. Hiyo inaleta tofauti gani kwa mwaminio wa kweli, watapindua bunduki ngapi? Amina. Mungu ameshika hatamu mikononi Mwake. Amina. Na

popote inapofikia wakati wetu wa ku—kuondoka hapa, iwe ni kwa, kwa njia yoyote ile tuendayo, hakuna kitu, si mauti, hakuna kitu kingine kinachoweza kututenganisha na Mungu. Tuna Uzima wa Milele, hatuwezi kuingia katika hukumu, maana Kristo alisema hivyo: tayari tumepita kutoka mautini kuingia Uzimani.

⁴⁷ Sasa, huko Yerusalemu, mwanzoni mwa somo letu usiku wa leo, ilikuwa ni miaka mitatu na nusu ya ajabu sana. Walikuwa na uamsho. Matarajio makubwa sana yakiwangoja watu, juu ya Mtu ambaye ulimwengu na kanisa vilimkataa: Bwana Yesu. Alihesabiwa kuwa mlokole. Nasi tungeita, leo hii, kama tungeiweka katika yale maneno, leo hii, Yeye alikuwa mtakatifu anayejifingirisha. Hakukubaliana kabisa na theolojia yao. Na hata hivyo, Mungu alithibitisha ya kwamba alikuwa pamoja Naye.

⁴⁸ Petro alisema katika Matendo 2, alisema, “Enyi watu wa Israeli, mlipaswa kujua jambo hili. Kwa maana huyu Yesu wa Nazareti alikuwa mtu aliyethibitishwa na Mungu kwenu, kwa ishara na maajabu ambayo Mungu aliyafanya kwa mkono Wake katikati yenu, ambapo ninyi pia ni mashahidi. Mlipaswa kujua hilo, lakini,” kasema, “ninyi, kwa mikono miovu mmemsulubisha Mfalme wa Uzima. Basi Mungu amemfufua, na sisi tu mashahidi.” Ndivyo ilivyo. Mungu alithibitisha ya kwamba huyo alikuwa ni Mwanawe mpendwa, kwa ishara na maajabu aliyofanya, akionyesha ya kwamba Mungu alikuwa pamoja Naye.

⁴⁹ Ninataka kuwaulizeni jambo fulani, waaminio, na hasa sana kwa...ndugu zangu wahudumu hapa nyuma. Wakati wowote kanisa, katika miaka elfu mbili iliyopita, limewahi kuwa na uamsho, ama wakati wowote ulimwenguni ambapo kanisa lilipata kuwa na uamsho, kulikuwako na ishara na maajabu yaliyofuatana na huo uamsho. Naam, bwana. Ishara za Mungu wa Kimbinguni akiishi ndani ya watu, ambazo huwapa watu mtazamo. Tuna tumaini gani, isipokuwa tujue kwamba kuna kitu Fulani cha Kimbinguni?

⁵⁰ Kila mtu anajaribu kutazama ng’ambo ya pazia la wakati. Unajua unatoka mahali fulani, unaenda mahali fulani, kwa hiyo inahitaji mtazamo mdogo ng’ambo ya pazia la wakati. Musa alitaka kuiona. Mungu akamruhusu kuiona. Kwa hiyo tunaweza kuiona pia, Kristo, Yule aliyefufuka.

⁵¹ Sasa, kanisa lililotoka katika ushirika wao pa—pamoja na kanisa kuu la Kiyahudi la Othodoksi wakati huo, Baraza la wazee, nao walijiondoa wenyewe, nao walikuwa wamemfuata Bwana Yesu, haidhuru watu waliandikaje Jina Lake kwa chuki kama mwana haramu, walitambua ya kwamba Mungu alikuwa ndani Yake.

⁵² Alisema, “Kondoo Wangu wanaijua sauti Yangu.” Mnaona, walikuwa wa kiroho ndani, na walipomwona, walitambua ya kwamba Yeye alikuwa tofauti na hao makuhani, na waalimu, na kadhalika. Kwa hiyo wakamfuata popote alipokwenda. Walimpenda.

⁵³ Hawakuweza kumwelewa. Alikuwa Siri, hata kwa Mitume. Hakuna aliyeweza kumwelewa, kwa sababu kulikuwa na Watu wawili waliozungumza wakati wote. Mwanadamu Yesu Kristo alikuwa akizungumza, naye Mungu alikuwa akizungumza ndani Yake, pia. Wakati fulani ilikuwa ni Kristo Mwenyewe; wakati mwingine ilikuwa ni Baba aliyeishi ndani Yake. Mnaliona? Yeye...hawakuweza kuelewa baadhi ya mambo ambayo angesema; alizungumza nao kwa mafumbo.

Yesu hatimaye alisema, alipokuwa akizungumza nao siku moja, jinsi, “Nalitoka kwa Mungu; nikaja ulimwenguni; nami ninarudi tena kwa Mungu.”

⁵⁴ Na kwa hiyo wanafunzi wakasema, “Sasa Wewe wasema waziwazi. Sasa tunajua, na tunaamini kwamba—kwamba Wewe wafahamu mambo yote, na kwa hili twasadiki ya kuwa Wewe ndiwe Mwana wa Mungu. Tunakuamini, sasa, kwa sababu Wewe unafahamu mambo yote; Mungu anakuonyesha mambo yote; wala huna haja mtu akwambie, kwa sababu Mungu anakuonyesha tu. Na hiyo ndiyo sababu tunaamini ya kwamba umetoka kwa Mungu.” Mnaona, baada ya wao... Mara baada ya kusulubiwa Kwake, Yohana Mtakatifu yapata, naamini mlango wa 15 ama 17, sikumbuki, 15, nafikiri.

⁵⁵ Vema, angalieni, sasa, walikuwa wamempenda na walimwamini, kwa sababu waliziona kazi Zake, ya kwamba Mungu alikuwa pamoja Naye na kulithibitisha Neno alilohubiri. Mnaona, mtu anaweza kuja na kusema lolote. Hilo ni neno la mwanadamu tu. Lakini Mungu anapokuja huku na kusema, “Hiyo ni kweli,” analithibitisha, basi afadhali uliamini, kwa sababu Mungu alisema hivyo. Unaona?

⁵⁶ Kwa hiyo alinena juu ya Mungu kuwa ndani Yake. Alisema, “Si Mimi nizitendaye hizo kazi; ni Baba Yangu akaaye ndani Yangu, Yeye huzitenda hizo kazi. Sifanyi neno kwa nafsi Yangu; yale tu ambayo Baba ananionyesha, hayo ninafanya.” Nao wakagundua, ya kwamba lolote Baba alilomwonyesha, Naye akawaambia, lilikuwa ni Kweli kabisa.

⁵⁷ Alisimama kwenye makusanyiko, akatambua walichokuwa wanawazia. Akasema, “Mbona mnahoji moyoni mwenu kuhusu hilo?” Mnaona? Naye akagundua mambo namna hiyo; wanajua yanatoka kwa Mungu. Ndipo akasema ya kwamba mambo aliyofanya, na jinsi Baba alivyomwonyesha, naye akagundua kila kitu alichosema kilikuwa ni kweli. Kwa hiyo hiyo ilikuwa ishara kwa Myahudi, kwa vyovyote vile.

⁵⁸ “Akiweko kati yenu mtu ambaye ni wa kiroho au nabii, Mimi Bwana, nitajidhihirisha Mwenyewe kwake katika maono, nitasema naye katika ndoto. Na yale nabii huyu asemayo, yakitukia, basi msikieni, kwa maana niko pamoja naye. Lakini yasipotimia, basi msimsikie, sijazungumza naye. Kwa uwongo tu katika mwili, sijamsikia, au sijakuwa pamoja naye.”

⁵⁹ Lakini ilikuwa ni ishara, nao waliona ya kwamba Mungu alikuwa akijidhihirisha Mwenyewe kwa njia ya Kristo. Na hivyo ndivyo Maandiko yalivyosema hasa, “Mungu alikuwa ndani ya Kristo, akiupatanisha ulimwengu na nafsi Yake.”

⁶⁰ Sasa, angalia, ndipo ukaja wakati wa kusikitisha, ya kwamba huyu Mtu mkuu, wa ajabu ambaye angeweza kusema na wafu, nao wangefufuka tena. . . Si wafu wote, Yeye alizungumza tu na watatu wao, kama ilivyoandikwa katika Maandiko, na hao watatu wakafufuka, kwa sababu tatu ni ushuhuda, u—ushahidi. “Kinywa cha mashahidi wawili au watatu, kila neno huthibitishwa.” Na kila wakati, Yeye alisema Baba alikuwa amefanya hilo, Baba alimwonyesha la kufanya.

⁶¹ Sasa, nao walikuwa wamemwona Mtu Ambaye angeweza kuwafufua wafu, na hata hivyo afe. Sio tu kufa kifo cha kawaida, awe mgonjwa kisha afe, lakini angesimamishwa na kudhihakiwa, Mtu ambaye angeweza kutambua mawazo yao na kuwaambia watu kile walichokuwa wakifanya, kisha ilipofikia kwenye majaribio, yale majaribio, alifungwa kitambaa kichwani Mwake, nao wakampiga kichwani kwa fimbo, na kusema, “Wewe ni mtabiri; twambie ni nani aliyekupiga; tutakuamini sasa.”

⁶² Kisha wakanyoosha mkono, wakavuta ndevu kutoka usoni Mwake, Mtu wa Kiungu. Hiyo ingewezekanaje? Nawazia wafuasi Wake walisema, “Vema, kwa nini asifanye tu jambo fulani kuhusu hilo?” Vema, kama angalifanya jambo fulani juu yake, mimi na wewe tungekuwa katika hali mbaya sana usiku wa leo. Asingeweza kufanya lolote kulihusu, kujiokoa Mwenyewe na kuwaokoa wengine, ilimbidi ajitoe Mwenyewe.

⁶³ Kwa hivyo hakufanya mzaha na karama na uwezo Wake. Walimpiga kichwani, wakasema, “Sasa, tuambie ni nani—nani aliyekupiga.” Ndipo alipokuwa msalabani. . . Angeweza kuwaokoa wengine na kuyatuliza mawimbi ya bahari. Na huku ameshikwa na homa kali, Naye yuafa, Damu ikimtoka, nao Wayahudi wakasema, “Sasa, kama wewe ni Mwana wa Mungu, utuonyeshe mwujiza. Utufanyie kitu fulani. Shuka msalabani, nasi tutakuamini kuwa ni Mwana wa Mungu. Tutakuamini ikiwa utatoka msalabani.”

⁶⁴ Mnaona? Huyu roho mkosoaji, jinsi ambavyo Mungu, jinsi anavyoruhusu tu mambo hayo yatendeke hivyo. “Kwamba ninii. . . huwapumbaza wenye hekima na busara na atawafunulia watoto wachanga, watakaojifunza.” Huna budi

kusahau yote uliyowahi kujua, na uwe mtiifu kwa Roho wa Mungu, ndipo Mungu anaweza kuendelea kukufundisha.

⁶⁵ Usijaribu kuondoka na kupata elimu hizi zote kubwa na misaada ya masomo upate kumjua Mungu. Humjui Mungu kwa misaada ya masomo; unamjua Mungu kwa imani. Unamwamini, naye Mungu anajidhihirisha Mwenyewe kwako. Ninapenda hilo, nanyi je? Ameifanya rahisi sana, nyenyekevu sana.

⁶⁶ Sasa, ni nyenyekevu sana na ni rahisi sana, hata watu wenye hekima hawawezi kulielewa. Imerahisishwa sana, mpaka wenye busara hawaipati. Wanajaribu kuifanya iwe ngumu kwa kanisa. Wanajaribu kuifanya iwe mambo mengi sana ya kutakasa unayopaswa kufanya, na kuacha *hili*, na kufanya *hili*, na *haya* yote, *yale*, na *mengineyo*. Na, mbona, sivyo kabisa; liamini tu, na ulikubali na hilo latosha. Mungu huingia ndani ya moyo, Naye anashughulikia mengine yote. Kama Yeye anaweza kupata ninii—ninii. . . moyoni mwako, apate nafasi moyoni mwako, basi yaliyosalia yatajishughulikia yenyewe. Napenda hilo.

⁶⁷ Angalia, basi angewezaje Mtu wa Kiungu, Ambaye walidhani ndiye Mfalme aliyekuwa yuaa, Mkombozi wa Israeli, kwamba Mtu huyo, kujinyenyekeza Mwenyewe, kuwaacha Mataifa wachafu wampige kichwani, wala asiwaambie lolote? Kwa nini hakuonyesha nguvu Zake? Mungu ana nyakati na njia za kufanya mambo. Waling'oa ndevu Zake, wakamtemea mate usoni, ni tusi la namna gani. “Fanya kitu juu yake; wewe ndiye mfalme.”

⁶⁸ Alisema, “Ningeweza kumwomba Baba Yangu, Naye angenitumia Mimi majeshi kumi na mawili ya Malaika, lakini Ufalme Wangu si wa ulimwengu huu.” Unaona? Kasema, “Hamlielewi.”

⁶⁹ “Loo,” wakasema, “Mwondoshe mlokole kama huyu.” Nao wakampeleka huko juu na kumsulubisha, Naye akafa, wakamzika, na kumwondosha, na kumtia muhuri kaburini.

⁷⁰ Sasa, nena juu ya watu waliosikitika kulazimika kutoka nje na kukabiliana na ulimwengu tena, wakiisha kutoka makanisani mwao, wakiadini katika aina hiyo ya dini. Nao walitoka makanisani mwao, ndipo ikabidi warudi na kukabiliana na makanisa yao tena, baada ya kitu kile kile walichokuwa wameamini, inavyoonekana, kushindwa. Hapo ikaninii, wao. . . Ilionekana matumaini yote yalikuwa yamekwisha.

⁷¹ Mtu yeye yule waliyemdhania kuwa ndiye Nabii wa Kiungu, ama, Ma—Masihi, alikuwa ametumiwa vibaya sana mbele za watu, na mnyonge sana na asiyejiweza. Alipokuwa huko nje miongoni mwa watu alifanya kila namna ya ishara, lakini alipokuwa amesimama hapa mahakamani, hakujaribu hata kujitetea Mwenyewe, aliwaacha tu wote wampige kote, wakamwegemeza kwenye nguzo ya kucharazia, akaistahimili ile mijeledi ya mikia kadhaa, vidonge vikubwa vya risasi nchani

mwa ngozi yake, na kuupasua mgongo Wake nayo, wakati walipompiga mijeledi mgongoni Mwake; kamwe hakufungua kinywa Chake.

⁷² Wakampandisha mlimani, na kumsulubisha msalabani, wakamshusha na kumweka chini, nyama zikiraruliwa mikononi Mwake. Na hata alilia apate rehema. Hiyo ni kweli.

⁷³ Sasa, hebu ingiza mawazoni mwa watu: “Huyo angeweza kuwa Mwana wa Mungu, na angeweza kuwaacha watu wamtendee, na kumpondaponda kote, na kumfanyia hivyo?” Mnaona, kutokuyajua Maandiko ndiyo sababu waliyatenda . . . wao . . . ilikuwa. Sasa, tutaona katika dakika chache.

⁷⁴ Vema, walikuwa wamemzika, kwa hiyo, vema, Sabato ilikuwa imekwisha, ikaja siku ya kwanza ya juma, wakakesha kwa ajili ya Sabato. Petro akachukua nyavu zake za samaki na alikuwa anarudi kwenda kwenye biashara yake tena, kuvua samaki. “Vema, nafikiri nilikosea hata hivyo. Labda Jamaa huyo alikuwa mlokole.”

⁷⁵ Ninaweza kumwona Kleopa na rafiki yake wakisema, “Vema, na turudi Emau; yote yamekwisha. Mtu tuliye kuwa na imani naye sana kuwa Mtu halisi, wa kweli, wa Kiungu aliyetumwa kutoka kwa Mungu, Mtu wa Kiungu kweli, hata hivyo hapana shaka kweli ilikuwa, labda lile kanisa kubwa lilikuwa sahihi: ‘Hiyo ilikuwa telepathia ya kiakili; alikuwa akisoma mawazo yao.’” Mnaona?

⁷⁶ Wanadamu: “Labda kweli alikuwa mwana mizimu. Labda Yeye alikuwa tu ni mwana mizimu, na hiyo ndiyo sababu dunia ilitikisika na kadhalika, wakati Yeye alipokufia kule juu. Labda Yeye alikuwa vile tu kuhani alivyosema alikuwa, Beelzebuli. Kanisa lote . . . Labda hiyo ilikuwa ni kweli.”

⁷⁷ Basi akamchukua rafiki yake, akasema, “Twende zetu sasa, turudi Emau, nyumbani, nasi tutaanza kazi yetu ya useremala,” au chochote kile, “tuanze tena kujenga,” au chochote walichokuwa wanakwenda kufanya. Wamevunjika moyo kabisa, wakienda zao njiani, wamehuzunika, bila kujua kwamba Bwana Yesu mbarikiwa alikuwa amefufuka katika asubuhi hiyo ya Pasaka, naye alikuwa hai miongoni mwa watu.

⁷⁸ Ndugu, uhai wa mimea haumaanishi tu maua na kadhalika; unamaanisha ufufuo pia, katika hali hiyo. Amina. Wakati tu wa majira ya kuchipua, wakati maua ya Pasaka yanapochanua, kila kitu kizuri sana, mfano halisi wa asili; ufufuo hauna budi kuja katika majira ya kuchipua. Hiyo ndiyo sababu ufufuo uko katika majira ya kuchipua. Ufufuo wa kila kitu, na hakika Mfalme wa maumbile alifufuka . . . Muumba wa maumbile alifufuka pamoja na ufufuo wa maumbile mengine.

⁷⁹ Nao hawa hapa, wakienda zao kwenye makazi yao, wakitembea barabarani. Ningeninii tu . . . Ningependa kuwasikiliza, nanyi je, kwa dakika moja tu, msimame karibu,

muone walichokuwa wakisema? Nasikia mmoja wao akisema, “Vema, Kleopa, waonaje juu yake? Ninasikitika. Vema, nadhani itatubidi tukabiliane na yule mhubiri tena, tumwambie, ‘Nadhani tulikosea katika Mtu huyu.’ Jamani, sipendi kufanya hivyo; imani yangu ilijengwa kabisa ndani Yake.”

⁸⁰ Basi angalieni, walipokuwa wakinena juu Yake, wakizungumza juu Yake, Yeye alitokea. Hiyo ni njia nzuri ya kumleta karibu nawe: zungumza habari Zake wakati wote. Amina. Endeleza mazungumzo yako, sio juu ya nani, au, ambapo mchezo mwingine utatokea kwenye televisheni, au sinema nyingine itakayotokea, au ni nani atakayechaguliwa kuwa rais: nena juu ya Yesu.

⁸¹ Wakristo wanazungumza juu ya kila kitu isipokuwa Kristo siku hizi. Wanatoka, daima huwa na lundo la upuuzi na kila kitu wanachotaka kuzungumzia ama chochote kile, lakini kamwe hawazungumzi juu ya Kristo. Nena juu Yake; imba juu Yake. Mpende Yeye; mweke moyoni mwako na niani mwako mchana kutwa na usiku kucha.

⁸² Daudi alisema kuhusu...angezifunga sheria vidoleni mwake na kwenye besera, na hivyo Yeye angekuwa mbele zake wakati wote. Hiyo ndiyo njia: mweke mbele yako katika kumbukumbu, mawazo, sifa, maongezi. Yote unayofanya mweke Kristo mbele yako. Hiyo ndiyo njia ya kumweka karibu nawe.

⁸³ Walipokuwa wakizungumza juu Yake, alijitokeza jukwaani, pasipo kujulikana kwao. Wengi wa watu waliompenda kweli hawakujua kwamba alikuwa amefufuka katika wafu. Na kama hiyo ndiyo...kama hiyo siyo maana halisi ya neno hili usiku wa leo, sijui ni nini. Wengi wa watu wanaompenda Bwana Yesu kweli hawawezi kuelewa kwamba Yeye yuko hapa.

⁸⁴ Yuko kwenye jengo hili hivi sasa. Anaingia na kutoka kwa watu, Bwana Yesu aliyefufuka. Ni vigumu sana kwa watu kuona hilo. Angalieni, ninyi mnaoketi hapa katika viti hivi na vitanda na kadhalika, kama mngeweza kuona hilo, mngeninii...na kuliadini kwa moyo wako wote, na kulikubali Neno Lake, ungetoka hapa usiku wa leo mtu mkamilifu, mzima. Naam, kwa maana amefufuka katika wafu.

⁸⁵ Angalieni, akitembea pamoja nao, walimpenda, wala hawakujua, hawakujua ya kwamba alikuwa Ndiye. Mara nyingi amekuwa papo hapo pamoja nawe, na hapo labda, wakati ulipokuwa karibu sana kupata ajali, kitu kilitokea; hujui kilichotokea. Kitu fulani kikatendeka; huyo alikuwa ni Yeye. Wakati daktari alipokuja, akasema, “Huyo mtoto, sioni jinsi anavyoweza kuishi.” Na baada ya kitambo kidogo, huyo mtoto akapona; huyo alikuwa ni Yesu. Yuko pamoja nawe. Loo, ni ajabu jinsi gani.

⁸⁶ Hapa muda mrefu uliopita, maskini mwanamke mmoja aliyekuwa...Nakumbuka alienda kuishi chini ya kanisa langu;

angali huko sasa, Jeffersonville. Alikuwa katika kituo cha afya huko Waverly Hills, nao wakamleta huko chini, wakasema, “Daktari alisema hana budi kufa mara moja.” Walitaka kumpa, ninaamini siku kumi, majuma mawili ya kuishi, ugonjwa wa kifua kikuu. Nami nikashuka kwenda kumwona.

⁸⁷ Wakaniita kule chini, yapata, imekuwa yapata miaka minane iliyopita ama kumi, kabla tu sijaja Phoenix mara ya kwanza. Basi nikashuka kule na nilikuwa nikimwomba huyo mwanamke. Alikuwa na watoto wadogo watano hivi. Nami nilikuwa nikiomba pamoja naye usiku huo, basi nilipokuwa nimeomba na kusimama, nilimwona, hata akiwa na nywele zenye mvi zilizotiwa rangi. Alikuwa...nywele zilikuwa za hudhurungi iliyokoza. Nami nikamwona akiwa na nywele zenye mvi zilizotiwa rangi. Watoto wake wakiingia ndani, wakipeana mikono naye, miaka mingi baadaye. Nami nikasema, “Dada, BWANA ASEMA HIVI; utaishi.”

⁸⁸ Akaanza kulia. Akasema, “Kasisi Branham, jambo fulani limetukia moyoni mwangu.” Akasema, “Ni—ninajisikia tu kwamba nitaishi. Kitu kinaniridhisha tu, nitapona.”

Nikasema, “Naam, kwa kuwa ni BWANA ASEMA HIVI.” Nilirudi juu, nikawaambia kanisani.

⁸⁹ Kulikuwa na mtu aliyeishi jirani yangu, rafiki mzuri sana, naye alipenda kutengeneza bidhaa za ngozi. Jambo lingine, alinitengenezea kitabu hiki cha mfukoni, ambacho nimekuwa nacho...nimekibeba miaka kumi, basi akakitengeneza kwa ngozi ya paa ambayo nilijipatia. Kina picha ya maskani yangu, ndani, kina samaki *hapa* na kichwa cha paa *hapa*. Kwa hiyo akanitengenezea maskini kijitabu hicho cha mfukoni, nami nimekibeba katika ukumbusho wa jambo hilo, kwa muda mrefu sana.

⁹⁰ Kafiri kamili, wa kupindukia, mwanasayansi, alifanya kazi kwenye bohari ya serikali. Hakuamini kulikuwa na kitu kama Mungu. Kasema, “Mtu yeyote ambaye aliamini hivyo ni mwendawazimu.” Akasema, “Wewe ni...”

⁹¹ Ni—ninaweza kuelewa kwa urahisi, jinsi watu wanavyoweza kuingiza hilo niani mwao. Asubuhi ya leo, nikisimama katika ofisi ya mfanyabiashara, hapa katika mji huu, pamoja na wahudumu fulani, jinsi walivyozungumza kuhusu jinsi Uislamu, huko Afrika, unavyoenea. Angalieni, Waislamu ishirini na watano kwa Mkristo mmoja, hilo ndilo shinikizo. Kwa nini? Uislamu umeunganishwa pamoja, umoja. Wanaamini kwamba Korani imevuviwa.

⁹² Sisi Wakristo, jambo la kwanza, tumetenganishwa kati ya Wakatoliki na Waprotestanti. Mkatoliki anasema, “Biblia imevuviwa, lakini kanisa Katoliki liko juu ya Biblia.”

Mprotestanti alisema, “Vema, imevuviwa kadiri ninavyoamini. Hayo mengine hayajavuviwa.”

⁹³ Kuzozana, kupigana, kubishana, kutengana, loo, ni jambo la kusikitisha. Hakika nina furaha Mungu alinishika kabla kanisa halijanishika (Hiyo ni kweli. Naam, bwana.), kwamba Mungu alinishika kwanza, kwa sababu labda ningekuwa kafiri, ninapooa watu wanaojiita Wakristo na—na kanisa na kadhalika, na kila mmoja akitaka kuvuta visubi wadogo na kadhalika kutoka kwa mmoja hadi kwa mwingine, na kutengana, inavyoonekana, bila kuwa na imani. Hakika.

⁹⁴ Sasa, mtu huyu alikuwa kafiri kabisa. Ndipo mtu fulani akatoa habari kesho yake ya kwamba nilisema hivyo kuhusu huyo mwanamke. Sikuwa nimetoka nje kufanya ibada bado. Nilikuwa nikifanya doria kwenye nyaya za juu na nguo zangu zimechakaa. Nilipanda baiskeli yangu kuukuu nikaenda kuchukua vyakula dukani, ndipo ikanibidi kupiga kona ambapo mwanamke huyo aliishi, bloku mbili tu chini ya pale nilipokuwa. Basi huyu hapa kafiri anakuja akitembea barabarani. Ndipo akazungumza nami.

Nikasema, “Habari za asubuhi, bwana.”

Naye akasema, “Aloo, mhubiri.” Kasema, “Hebu kidogo, nataka kuzungumza nawe.” Akasema, “Kwani huna aibu?”

Nami nikasema, “Kitu gani?”

Akasema, “Kumwambia maskini mama huyo anayekufa mle ndani, ya kwamba ataishi, kuwajenga watu hao chini ya tumaini la uongo kama hilo.”

Nikasema, “Vema, kamwe sikuwajenga chini ya tumaini la uongo.”

⁹⁵ Akasema, “Vema, yuafa.” Kasema, “Mume wake anafanya kazi pamoja nami huko nje serikalini.” Kisha kasema, “Aliniambia ya kwamba ulikuja huko jana usiku, na, ama, ilikuwa ni hivi majuzi usiku, ukamwombea. Naye... nawe ukamwambia kuwa atakuwa mzima na kuishi akawa mwanamke mzee.”

Nikasema, “Hiyo ni kweli. Sikuwahi kufanya hivyo; Mungu alifanya hivyo.”

Akasema, “Upuuzi,” akasema, “jionee aibu. Unapaswa kuwa muungwana vya kutosha kutowajenga watu chini ya vitu kama hivyo, vya uongo namna hiyo.”

Nikasema, “Hiyo si uongo.”

Akasema, “Achana na mambo kama hayo.” Akageuka akaondoka.

⁹⁶ Ndipo nikawazia, “Vema, sawa.” Nami nikaendelea, nikanunua vyakula vyangu, nikarudi. Takriban siku mbili au tatu baada ya hapo...Alikuwa na maskini mke mzuri aliyekuwa mwaminio, na kwa hivyo mimi...mke wangu alimjua vizuri sana, alisema alikuwa mwanamke mzuri. Naye

alikuwa mfuasi wa kanisa la Kikristo. Kwa hiyo mke wangu akaniambia nilipoingia, akasema, “Vema, yule Bibi Andrews ni mgonjwa sana, Billy.” Kasema, “Unapaswa kwenda ukamwone.”

⁹⁷ Nikasema, “Sawa.” Nikasema, “Mumewe ni yule kafiri,” Nikasema, “I—inanibidi kutembea kwa uangalifu.” Kwa hiyo nikasema, “Nitaenda na kumwuliza ikiwa ninaweza kumletea kuni na makaa ya mawe, na labda atauliza... labda ataniuliza kama mimi... anataka nimwombee.”

Na kwa hivyo nikaenda kule, nami nikasema, “U hali gani, Bw. Andrews.”

Akasema, “Aloo, mhubiri.”

Nami nikasema, “Nasikia una mke mgonjwa.”

Kasema, “Naam, ninaye, lakini nina daktari mzuri pamoja naye.”

⁹⁸ Nikasema, “Naam, bwana. Nilitaka tu kukuuliza Bw. Andrews, kwa kuwa sisi ni majirani hapa karibu sana, kama ningeweza kukusaidia kuleta makaa au kukimbia dukani kununua vyakula, chochote, ni—ningekufanyia.”

⁹⁹ Kasema, “Aa, vema, asante sana.” Lakini akasema, “Tunaye daktari mzuri pamoja naye; kila kitu kitakuwa sawa.” Akaniambia alikuwa ni daktari gani jijini.

Nami nikasema, “Yeye ni mtu mzuri.” Nikasema, “Nampenda sana.”

“Naam, tumeidhibiti hali yake,” kasema, “ana ugonjwa wa kidole tumbo,” kisha kasema, “itakuwa sawa,” kasema, “anaigandisha kabisa; itakuwa sawa.”

¹⁰⁰ Nikasema, “Asante, Bw. Andrews, hakika ninatumaini hivyo. Kama naweza kuwa msaada wowote kwako, ninaishi jirani, nipigie simu tu.” Kafunga mlango, akarudi huko, kwa namna fulani hajali.

¹⁰¹ Vema, kesho yake daktari akaja, akasema, “Itabidi tumpeleke hospitalini; anavimba vibaya sana.” Kasema, “Itabidi tumpeleke hospitalini na kufanya upasuaji.”

¹⁰² Kwa hiyo wakampeleka hospitalini, na walipoipima damu yake, wakagundua hakuwa na kidole tumbo. Kwa hiyo wakatuma mtu Louisville kumleta mtaalamu. Nao wakampata mtaalamu kule, naye huyo mtaalamu akamchunguza, basi alipofanya hivyo alisema, “Ana kati ya saa nne na sita za kuishi. Kuna donge la damu karibu sana na moyo; hilo ndilo linalovimba.” Kasema, “Amekwisha; hamna lingine.”

¹⁰³ Kwa hivyo mke wangu akaniambia kesho yake asubuhi akasema, “Bibi Andrews yuafa, Billy.” Kasema, “Nilisikia tu kwamba ana donge la damu. Muuguzi, mmoja wa wale wauguzi, rafiki, akapiga simu, kasema, ‘Yeye ni—ni mahututi,’ kasema, ‘tayari amepoteza fahamu.’”

¹⁰⁴ Nikasema, “Ni vibaya sana, Meda, nachukia kusikia hilo. Maskini huyo,” nikasema, “tutamwombea tu.” Kwa hiyo tukaomba, nami nikaendelea nikaanza kwenda kazini.

Na kidogo kulikuwa na mvua ya manyunyu, nami nilikuwa nikitoka nje kupitia shambani. Kitu fulani kikaendelea kusema, “Geuka urudi nyuma. Geuka urudi nyuma.”

¹⁰⁵ Kwa hivyo nikawazia, “Vema, nitageuka nirudi.” Kwa hivyo nikarudi, nikapiga simu na kuinakili kama hali mbaya ya hewa, kwa hivyo sikuweza kufanya kazi, kwa ajili hiyo tu, kwa sababu nilijua Bwana alitaka jambo fulani. Na kwa hiyo, muda si muda mwajua, nikaketi pale, kisha nikaitenganisha maskini bunduki yangu, nami nilikuwa nikiisafisha.

¹⁰⁶ Basi muda si muda mwajua, huyu hapa Bw. Andrews anakuja nyumbani, akitembea, kofia yake imeyafunika masikio yake, akabisha mlango na kusema, “Bibi Branham,” kasema, “hivi Mhubiri Branham yuko hapa?”

Kasema, “Naam, Bw. Andrews, mbona usiingie?” Basi akaingia.

Nikasema, “Aloo, Bw. Andrews; jitwalie kiti.” Nikaendelea tu kuishughulikia bunduki yangu, mwajua.

Naye akasema, “Um, uh, Mhubiri.”

Nikasema, “Naam, bwana.”

Akasema, “M—mke wangu yu mahututi. Ulisikia habari zake?”

¹⁰⁷ Nikasema, “Naam, nilisikia alikuwa yuafa, Bw. Andrews.” Nikasema, “Ni vibaya sana.” Nikasema, “Bila shaka, una daktari mzuri sana huko nje.” Kisha nikasema, “Na—natumai tu ataendelea vizuri.” Nikaendelea tu. . .

Akasema, “Vema,” kasema, “tulipata mtaalamu; unafahamu hilo?”

Nikasema, “Naam, ninasikia mlimpata, Bw. Andrews, nilisikia ilikuwa ni donge la damu karibu na moyo.”

Kasema, “Naam,” kasema, “hiyo ni kweli.” Kasema, “Jamani,” kasema, “yuko mahututi sana.”

Nikasema, “Naam, bwana, hakika hiyo ni mbaya sana.”

¹⁰⁸ Nikawazia, “Litolee jasho. Ulinifanya kutoa jasho, kwa hivyo sasa wewe toa jasho kidogo.” Kwa hivyo nikaendelea tu kuisafisha bunduki yangu, nikamwacha atoe jasho kidogo. Kwa hivyo nikaendelea tu kuisafisha bunduki yangu, nikiichungulia namna *hiyo*. Ilikuwa safi, lakini nilimtaka tu, achukue muda kidogo, kwa hivyo nikaendelea kuichungulia namna *hiyo*.

Naye akasema, “Mhubiri,” akasema, “unajua nini?”

Nikasema, “Ati nini, Bw. Andrews?”

Akasema, “Nashangaa kama ungeweza kumsaidia kidogo.”

Nami nikasema, “Unamaanisha nini?”

Akasema, “Unajua, um . . .”

Nikasema, “Unataka kusema, kumwombea?”

Akasema, “Naam.”

¹⁰⁹ Nikasema, “Nilidhani huamini kitu kama hicho.” Mnaona? Nikasema, “Nilifikiri uliniambia chini ya juma moja lililopita, pale chini pembeni, hata hukuamini kuwa kuna Mungu.”

Akasema, “Vema,” akasema, “wajua . . .”

¹¹⁰ Nikawazia, “Naam, wakati ukifika, utaamini. Hiyo ni kweli, iache tu ifike karibu vya kutosha mlangoni pako wakati mmoja, utaamini.” Nami nikasema yeye ni . . . “Vema, sawa, Bw. Andrews.”

Kile yeye . . . Akasema, “Je, wa—waweza kwenda ukamwombe?”

Nikasema, “Ninataka kukuuliza jambo fulani, Bw. Andrews.” Nikasema, “Vipi wewe kupiga magoti hapa pamoja nami, tumwombe papa hapa.”

Naye akasema, “Vema,” akasema, “Ka—karibu sijui la kufanya.”

Nikasema, “Wewe piga magoti tu hapa; nitakuelekeza.”

¹¹¹ Na hivyo akainama hapo chini. Nikasema, “Sasa inua mikono yako.” Naye akai- . . . Nikasema, “Jambo la kwanza, kutoka kwenye kilindi cha moyo wako, sema, ‘Mungu, unirehemu mimi mwenye dhambi.’” Kwa hiyo nikamwingiza katika maombi, naye akaanza kulia, kwa hiyo, loo, jamani, tulikuwa na . . .

¹¹² Akasema, akasimama, akapangusa macho yake; akasema, “Vema, mhubiri, u—u—unafikiri sasa atasaidika?” Nikasema . . . Akasema, “Ungependa kwenda huko?”

¹¹³ Nami nikasema, “Naam, nitaenda nikamwone.” Basi nikamwambia Meda, “Vaa koti lako.” Tukaenda huko nje, na alipofanya hivyo, hakututambua. Amevimba tu juu ya macho yake, na midomo yake imepinduka.

¹¹⁴ Kwa hivyo, maskini nesi, nilipoingia, alisema, “Njoo, Ndugu Branham.” Akanipeleka kule juu. Nami nikapiga magoti, nikamwombea, nikaweka mkono wangu juu yake, nikasimama pale kwa muda kidogo.

Mke wangu akasimama pale, naye akasema, “Unaona chochote?”

Nikasema, “Hapana mpenzi, sioni.”

¹¹⁵ Tukatoka nje, huko chini mahali watoto wachanga walipokuwa na kuangalia kwenye wodi ya uzazi pale, mwajua, ambapo watoto wachanga wote wamelala. Alikuwa akizungumza juu yao. Nikarudi kwa Bibi Andrews tena;

nilipoingia tu mlangoni, nikaliona. Loo, jamani, mbona, nikasema, “Mpenzi, litaisha. Usijali; Mungu amesikia.”

Ndipo nikaenda nyumbani. Bw. Andrews akaja huko, akasema, “Unaonaje juu yake, mhubiri?”

Nikasema, “Ataishi.”

Akaanza kulia, jamani. Naye akapaza sauti, “Ataishi.”

¹¹⁶ Nikasema, “Usijali; Mungu ameishasema kwa ono lile lile alilomwambia yule mwanamke kule chini ataishi, na sasa ameamka, kule chini, yule mwanamke,” nikasema, “sasa, Bibi Reece sasa,” nikasema, “sasa, ataishi pia.”

Ndipo akasema, “Loo, nina furaha sana, mhubiri.”

Katika dakika chache simu ikalia, naye akaenda huko. Kasema, “Njoo kwa mkeo mara moja; yuafa.”

Basi akaja akaniambia, nikasema, “Je, unaamini niliyokwambia?”

Akasema, “Vema, mhubiri, nataka kuamini,” kasema, “lakini wananiambia yuafa.”

Nikasema, “Aha, hayo hayaleti tofauti hata kidogo yale wasemayo.” Nikasema, “Mungu anapozungumza lolote, halina budi kuwa hivyo tu.”

Kwa hiyo akasema...kwa hiyo muda si muda mwajua, akasema, “Loo, siwezi kwenda kuona hayo.”

Nikasema, “Kuona nini?” Nikasema, “Bado unafikiri atakufa, sivyo?”

Akasema, “Ningali nina wasiwasi sana.”

Nikawazia, “Hilo ni zuri kwako sasa hivi, unaona, kulitolea jasho kweli kweli.”

¹¹⁷ Basi achilia tu; na muda si muda mwajua, simu nyingine ikaja; wakamwita upande wa pili wa barabara. Huyu hapa anakwenda kule, kisha akarudi. Ndipo akasema, “Sina budi kwenda hospitalini mara moja.” Kwa hivyo huyo akaenda hospitalini.

Nami...Meda akasema, “Unaonaje kuhusu hilo?”

¹¹⁸ Nikasema, “Mbona, usijali hilo. Mungu amesema hivyo tayari; hilo latosha.” Nikasema, “Ikiwa mwanamke huyo hatanipikia sambusa ya tofaa katika siku tatu kutoka sasa, nami nitakuwa nimeketi kwenye ukumbi ule na kuila, basi mimi ni nabii wa uongo.” Hiyo ni kweli. Angeweza kweli kupika nzuri pia. Kwa hiyo ni—nilijua hilo; kwa hiyo nikamwambia... nikawaambia pale pale hospitalini, nikamwambia nesi hivyo. Nikasema, “Ataniokea sambusa katika siku tatu kuanzia sasa. Ikiwa sivyo, basi ni—nitaondoka hudumani.” Hiyo ni kweli. Nikasema, “Kwa sababu ni kweli kabisa.”

¹¹⁹ Nanyi mwajuaje, alirudi kupitia uwanjani katika dakika chache, huku kamasii ikitoka puani mwake, naye alikuwa akirukaruka na kuyumbayumba namna *hiyo*. Akasema, “Mhubiri, mhubiri, kisia kilichotokea.” Kasema, “Nilikwenda huko kumwona, basi wakati nilipofika huko,” kasema, “kitu *fulani* kilikuwa kimeachilia,” kasema, “maji yote yalikuwa yamemtoka, naye alikuwa ameketi kitandani, akasema alikuwa na njaa. Nami nikamwita yule nesi.” Kisha kasema, “Walimletea supu tupu ya nyama, naye akasema, ‘Ondoeni kitu hicho; nataka supu iliyo na nyama na yenye kabeji.’” Akasema, “Yeye ni mzima na amepona.” Yu hai leo. Na Mungu wa Mbinguni, Ambaye alitazama chini. . .

¹²⁰ Yapata juma moja baadaye akanitengenezea kile kitabu cha mfukoni ambacho nimebeba tangu wakati huo mfukoni mwangu, kote ulimwenguni. Hiyo ni kweli; huo ni ukweli; Mungu Mbinguni anajua hilo. Yu hai usiku wa leo, kwa nini? Maana Yesu yu hai, yeye yu hai pia. Mungu alisema hivyo. Hiyo ni kweli.

¹²¹ Yesu, alipozungumza nao, alianza kuwafunulia. . . Angalieni, jambo lile lile. . . Walisema. . . Yeye alisema, “Kwa nini mmehuzunika?” Wakristo hawapaswi kuhuzunika; wanapaswa kuwa na furaha, furaha ya kweli, kushangilia. Alisema, “Mbona mmehuzunika sana?”

¹²² Yeye. . . wakasema, “Wewe ni mgeni tu, wala hujui ya kwamba Yesu wa Nazareti, Nabii, tuliyemtarajia kukitwaa kiti cha enzi cha Daudi. . .?” Kasema, “Sote tulimwamini. Yeye alifanya ishara kuu na maajabu mbele yetu, na jinsi Yeye alivyokuwa Nabii mkuu. Ndipo wakamsalimisha. . . watu wakamsalimisha kwa Pilato, nao wakamsulubisha, wakamzika.” Kisha kasema, “Leo ni siku ya tatu tangu yalipotendeka mambo hayo.” Kasema, “Wanawake kadha wa kadha wa kwetu walikwenda kaburini, pengine kuweka maua juu yake, ama chochote kile,” na kusema, “walisema kaburi lilikuwa tupu; nao wakaona ono lililowaambia kuwa amefufuka katika wafu.” Kisha kasema, “Vema basi, bila shaka tunaamini hiyo ilikuwa hadithi ya kipumbavu.” Kisha kasema, “Halafu,” kasema, “mmoja zaidi aliyekuwa pamoja na kundi letu, alisema ya kwamba aliona kitu fulani kulihusu.”

¹²³ Ndipo akatangulia, na kusema, Yeye akaanza. . . Tazameni, Yesu hakuanza kubishana nao wala kuzungumza. Alisema. . . Angalieni yale aliyofanya: alienda moja kwa moja kwenye Neno. Ndivyo hivyo. Ndugu, Neno la Mungu: hilo ndilo kiini na msingi. Kwa kuwa wokovu na uponyaji wote, umo katika Neno, si hisia zako, si kile unachowazia juu yake, bali kile Mungu amesema juu yake. Amina. Loo, laiti ningalikuwa na kibandiko, hata ningeweza kukibandika hicho moyoni mwako, ambapo kisingeweza kuondoka kamwe.

¹²⁴ Leo hii, nilikuwa nikisoma sehemu ndogo ya Maandiko, Yoeli. . . Amosi 8:11, ambapo ilisema, “Kutakuwa na njaa, si ya mkate, au, ya mkate na maji, bali ya kulisikia Neno la Mungu; kwamba watu wangetoka bahari hadi bahari, kutoka mashariki kutoka magharibi, huku na huku, kila mahali, wakitafuta. . . wakilitafuta Neno la Mungu wasilipate.” Ikiwa hilo halilingani na taifa hili kwa wakati huu, sijui linalingana wapi. Hiyo ni kweli. Hatuhitaji mkate; tunayo mingi. Tuna chakula kingi, nguo nyingi za kuvaa, nyumba nzuri za kuishi, na kila kitu; lakini kuna njaa ya kulisikia Neno la Mungu. Mtu hajui cha kuamini. Hiyo ni kweli.

¹²⁵ Nyote mmechanganyikiwa; mmoja anasema *hivi*, na mmoja anasema *vile*, na mmoja anasema *hivi*, na mmoja anasema jambo lingine. Wekea msingi mawazo yako juu ya BWANA ASEMA HIVI. Mungu atalithibitisha.

¹²⁶ Yesu alikwenda moja kwa moja kwenye Neno na kuanza kulimiminia Neno ndani; kasema, “Enyi msiofahamu na wenye mioyo mizito kufahamu.” Akarudi katika Agano la Kale na kuanza kuthibitisha jinsi Kristo anavyopaswa kuteswa na kufufuka siku ya tatu.

¹²⁷ Basi wakafika mahali padogo walipokuwa wakienda, kwa hiyo wakaingia kwenye mkahawa. Kwa hiyo akafanya kama anataka kuendelea mbele. Uliwahi kuwa na wakati. . . ? Labda maskini mtu huyu aliyelala hapa akiteseka kwenye kitanda hiki, amefanya kama atakupita; hatakupita. Unaona? Mwalike ndani.

¹²⁸ Labda maskini mtu huyu anayeketi hapa kwenye m—mkongojo, mtu anayeketi kwenye kiti cha magurudumu; Anaweza kutenda kama atakupita usiku wa leo, lakini hatakupita. Mwalike tu aje kwako, uone kitakachotokea. Mwalike tu ndani.

¹²⁹ Walisema, “Loo, karibu ndani; tunapenda tu kukusikia ukifundisha Neno. Tuliwasikia Mafarisayo wote na kadhalika, lakini kulikuwa na kitu fulani kuhusu mafundisho Yako kilichokuwa tofauti. Ingia ndani; hebu. . . tufundishe zaidi kidogo.” Basi wakaingia. Na mara wakiwa ndani ya mlango, labda maskini kibanda kidogo, haidhuru kilikuwa duni jinsi gani, lakini kamwe si duni sana Kwake kuingia.

¹³⁰ Haijalishi wewe ni maskini kiasi gani, jinsi ulivyo katika hali mbaya, wewe sio mbaya sana kiasi kwamba Yesu hataingia kwa mwaliko wako. Haidhuru umetenda dhambi kiasi gani, yale uliyofanya, mpe tu mwaliko, ataingia moja kwa moja na kufanya makao Yake. Hilo si linapendeza?

¹³¹ Vema, walimkaribisha ndani; basi akiisha kuingia, milango ilifungwa nyuma Yake, Yeye ataufungia ulimwengu wote nje. Sasa, kama wewe una ushirikina kidogo usiku wa leo, wa Uwepo wa Bwana, wakati mkutano ukiendelea, mwalike Yeye ndani ya moyo wako, halafu ufunge mlango na kutokuamini kwako

kwingine kubaki nje. Angalia kama Yeye hatajitambulisha Mwenyewe kwako.

¹³² Mara wakiwa humo ndani, wameketi mezani, labda mtumishi wa kike alikuja, nao wakaagiza chakula chao cha jioni. Basi walipokuwa wakikiweka mezani, bila shaka moyo Wake ukidunda, akiwatazama, nao wakimtazama, Yeye... Hawakujua. Sababu ya Biblia kusema macho yao yalifumbwa; ha—hawakulielewa. Walikuwa wameketi moja kwa moja pamoja Naye, wakitembea moja kwa moja Naye, wakizungumza moja kwa moja Naye, hapa wakila pamoja Naye, wala hawakujua Yeye alikuwa ni Nani.

¹³³ Basi rafiki, hiyo ni kweli kama iwezavyo kuwa leo. Hiyo ni kweli kama ninavyosimama kwenye jukwaa hili kwamba Yesu Kristo aliyefufuka yuko moja kwa moja katika jengo hili, akizungumza na watu binafsi sasa hivi, laiti ungaliweza tu kutambua ya kwamba hiyo ni Sauti Yake. Ninaomba ya kwamba atajidhihirisha Mwenyewe baada ya kitambo kidogo, na kuwathibitishia ya kwamba Yeye yuko hapa jengoni.

¹³⁴ Yesu hajafa, amefufuka kutoka kwa wafu. Naye yuko hapa duniani, akiendeleza huduma ambayo aliku... alipokuwa hapa duniani katika umbo la kimwili. Ameendeleza kupitia wanadamu kama alivyoahidi atafanya. “Mambo yale yale nifanyayo, ninyi nanyi mtayafanya.” Kuokoa, kufanya mapenzi ya Ba... Baba, hilo ndilo lililomleta. Naye yuko hapa usiku wa leo.

¹³⁵ Naye alipokuwa na hao wanafunzi mle ndani, wameketi mezani, aliwaangalia, akawaza, “Vema, mmenisikia nikifundisha Injili sasa. Mlinisikia nikihubiri leo, kwa hiyo naamini nitawajalia tu kujua ya kwamba Mimi Ndiye hasa.” Kwa hiyo akautwaa mkate, Naye akafanya tu tofauti kidogo na vile watu wengine walivyofanya, kwa hiyo wakatambua ya kuwa ilikuwa ni Yeye. Nayo macho yao yakafumbuliwa, nao wakatambua, Naye akatoweka mbele yao.

¹³⁶ Jamani, walikuwa mwendo wa Siku ya Sabato, wakienda kule, lakini hakika walirudi nyuma wenye miguu myepesi, wenye mioyo myepesi, wakiruka na kuruka-ruka na kumsifu Bwana. Walijua kwamba alikuwa amefufuka katika wafu. Wakarudi... hakurudi kubishania dini yao, sasa; walirudi wakiwa na jambo moja mioyoni mwao: Yesu amefufuka katika wafu.

¹³⁷ Hilo ndilo jambo usiku wa leo, sio kubishania dini, kubishania awamu mbalimbali, kubishania madhehebu mbalimbali ya kanisa, wakibishania taifa lingine, kile ambacho ulimwengu unapaswa kujua usiku wa leo: Yesu amefufuka katika wafu, Naye anaishi kati ya wanadamu. Amina. Si kubishana kuhusu kubainisha *hiki*, na kukata *hiki*, na kusogeza *hiki*, na *hiki* kuvuviwa; sahu tu, na umtazame Yeye, na kuamini

kwamba alifufuka katika wafu, Naye atajidhihirisha Mwenyewe kwako. Amina. Rahisi tu hivyo.

Unasema, “Vema, kama Malaika alikuwa akihubiri hilo . . .” Mungu hakuwaweka Malaika kuihubiri Injili. Aliwaweka wanadamu kuihubiri Injili.

¹³⁸ Kamwe hakuwaambia Malaika, “Nitakuwa pamoja nanyi na ndani yenu.” Aliwaambia wanadamu, “Nitakuwa pamoja nanyi na ndani yenu.” Kamwe hakuwaambia Malaika, “Mambo nifanyayo Mimi, ninyi nanyi mtayafanya.” Aliwaambia wanadamu, “Mambo nifanyayo Mimi, ninyi nanyi mtayafanya.”

¹³⁹ Injili huja kwa kulihubiri Neno. Mungu hujidhihirisha Mwenyewe kupitia kwa wanadamu. Amina. Macho pekee aliyo nayo Mungu duniani usiku wa leo ni yangu na yako, mikono pekee aliyo nayo ni mikono yetu: Mungu akitenda kazi ndani ya watu Wake; Mungu yuko katika maumbile; Mungu yuko katika Neno Lake; Mungu yuko ndani ya Mwanawe; Mungu yuko ndani ya watu Wake.

¹⁴⁰ Mungu yuko hapa sasa, amefufuka katika wafu, usiku baada ya usiku akijithibitisha Mwenyewe kuwa hai miongoni mwetu, akiwaleta wenye dhambi, wenye dhambi waliokufa, waliotengwa na Mungu, kuwafanya wamtambue Mungu, kuokoa nafsi zao, kuwajaza na Roho Mtakatifu, kuwaponya wagonjwa, kuafumbua macho ya vipofu.

¹⁴¹ Amkeni, enyi watu. Msichukuliwe huku na huku na kila upepo wa mafundisho, mkisema, “Siku za miujiza zimepita, na mambo haya ni ya wakati mwingine.” Msichukuliwe huku na huku; mwaminini Bwana Yesu aliyefufuka. Hayo yalikuwa ndiyo mafundisho yao kule nyuma alipofufuliwa na . . . kwenye asubuhi hiyo ya Pasaka. Lakini Yeye alikuwa hai, Naye yuko hapa usiku wa leo. Yuko hapa; usisahau hilo kamwe.

¹⁴² Endapo kamwe hamtakumbuka lolote ambalo nimewahi kuwaambia, nikumbukeni kwa jambo hili: kwamba Yesu Kristo Mwana wa Mungu alifufuka kutoka kwa wafu na yuko hai leo hii miongoni mwa wanadamu, akiwatafuta wenye dhambi, kuponya wagonjwa na wanaoteseka. Yeye ni yeye yule katika kila njia ambayo aliwahi kuwa na atakayokuwa; yeye yule jana, leo, na hata milele, Bwana Yesu, akiwatafuta wenye dhambi waliopotea.

¹⁴³ Je, umepotea? Ikiwa umeokoka, ni vizuri sana. Lakini ikiwa umepotea, Mungu ana maandalizi ya kukuokoa kwayo. Kitu kibaya sana ninachoweza kufikiria ni mtu aliyepotea. Nikiwa mwi—mwindaji, mimi huenda milimani . . .

¹⁴⁴ Dakika moja tu kabla ya kufunga sasa, halafu basi tutaanza kuwaombea wagonjwa, katika dakika moja tu. Ninajisikia itambidi Roho Mtakatifu kuwaita watu hapa, niwaombe.

¹⁴⁵ Sasa, nilipotea wakati mmoja msituni. Nilipanda kufikia karibu na mpaka wa Canada, ambapo nilikuwa. Nilidhani

nilikuwa bingwa sana wa mwituni kuwahi kupotea kamwe. Basi unapojiamini, naam, ndipo unapopotea; hapo ndipo unapopotea. Hapo ndipo Adamu alipopotea, alipojitumainia kutengeneza jani la mtini la kujifunika. Mnaona? Ilibidi aje kwa ustahilifu wa damu iliyomwagika.

¹⁴⁶ Na kila unapowazia, “Loo, ninaenda kanisani; mimi ni mwema kadiri ulivyo wewe, mhubiri.” Bila shaka u mwema, lakini je, u mwema kadiri Mungu anavyotaka uwe? Kwanza kabisa wewe si mwema, nami kwanza kabisa si mwema. Wema pekee ulio ndani yetu ni kile Mungu alichotufanyia kupitia kwa Yesu Kristo. Hiyo ni kweli. Naam, bwana. Sisi sote ni wenye dhambi, lakini njia pekee tunayoweza kuokolewa ni kwa kumkubali Bwana Yesu na msamaha Wake wa bure.

¹⁴⁷ Sasa, nilikuwa nimepotea kabisa. Nilimwambia mke wangu nitarudi. Nilimchukua; Billy alikuwa tu mtoto mchanga, jamaa mdogo wa takriban umri wa miaka mitatu, minne, naamini umri wa miaka mitano. Nasi tulikuwa huko mbali kwenye kilele cha Adirondack, karibu na mpaka wa Canada. Nasi tukaendesha gari kama maili ishirini na tano, thelathini kupanda kwenye maskini barabara ya magogo ya kale namna *hiyo*, ambapo walikuwa wamekata kiasi, kukata mbao zisizosagwa. Nasi tukaja kwenye kambi ya walinzi. Nilikuwa nimewinda huko kwa miaka mingi.

¹⁴⁸ Nilimwambia mke wangu nilikuwa ninaenda kuwinda dubu, ndipo nikasema, “Ninashuka hapa kuwinda paa, nami nitamchukua paa, nirudi; nitarudi ifikapo adhuhuri.”

¹⁴⁹ Akasema, “Nitakuwa nikikungojea.” Baridi usiku huo; ilitubidi kumchukua mtoto Billy na kumweka kati yetu, asiye akafa kwa baridi kali; Novemba baridi na matawi yalikuwa yakiganda, yakianguka kutoka mitini. Kulikuwa na kimbilio dogo, sehemu zingine za hicho kibanda zilikuwa zimefungwa. Mlima Tufani, mnara uliowekwa pale, nasi tulikuwa twende huko mbali kabisa huko nyuma katika sehemu hiyo nyingine ya nchi kuwinda.

¹⁵⁰ Kwa hivyo huyo mtu alikuwa atafungua hicho kibanda, naye angeweza kuingia mle, yeye na Billy wakae, wakati tukifanya hiyo safari na kuondoka; kwa hiyo, yeye akiwa tu ni mtoto, yeye mwenyewe, yapata umri wa miaka ishirini na mmoja, ishirini na miwili. Na kwa hiyo, usiku huo—usiku huo nusura tugande. Kwa hivyo, tukawasha moto mdogo na kutengeneza kitu cha kuegemea, na kwa hiyo basi kesho yake asubuhi nikaondoka kwenda kuwinda paa, kwa kuwa huyo mtu alipaswa kuja siku hiyo.

¹⁵¹ Na kwa hivyo, nikamwambia nitarudi adhuhuri. Basi nikashuka kuvuka hicho kilima kupitia vipande vya kuni. Nikarudi kupitia kando ya mgongo wa kilima, ndipo ni—nikaona paka mkia mfupi akipita, nami nisingeweza kumkaribia vya

kutosha kumpiga risasi kwa hiyo nikapanda juu ya kilima. Nami nikafuatilia kando nikaingia kwenye pango kubwa la dubu. Wala hapakuwapo na kitu mle; nikarudi, nikashuka kuelekea kwa majitu, wanayoita majitu: msitu mkubwa mle ndani maili baada ya maili, wote ni tambarare ya miti, namna hiyo, mle ndani, ni ngumu.

¹⁵² Kwa hiyo nikafika huko chini kabisa kandokando, ndipo nikamwona kulungu pale, jamaa mkubwa sana, nami nikampiga risasi huyo kulungu. Nilipomalizana na pale, ni—nikasema, “Vema sasa, angalieni hapa, ni baada ya saa sita, kwa hiyo sina budi kuharakisha.” Basi nikarudi, nikaanza kurudi *hivi*. Nami... Ikaja, dho—dhoruba ilikuwa inashuka, ukungu. Ukungu unapoingia msituni, mwindaji yeyote anajua huo ni wakati hatari. Ni vigumu kuuona mkono wako mbele yako.

¹⁵³ Naam, nilianza kutembea. Nikasema, “Sina budi kuharakisha.” Nami nikazunguka; nikaendelea kutembea, kutembea, kutembea, kutembea. Nikawazia, “Vema, jamani, kwani niligeukia wapi?” Ndipo muda si muda mwajua, ilitokea nilisimama, nikaangalia, nikawazia, “Vema, nimeona mahali hapa mahali fulani.” Nikatazama juu, na hapo nikamning’iniza paa wangu. Um-hum. Vema, nilijua nilikuwa nimezunguka mahali fulani. Kwa hiyo nikasema, “Sasa, sina budi kushika njia moja ya hakika.” Nami nikatembea tena, nikarudi mahali hapo mara tatu, moja kwa moja.

¹⁵⁴ Sasa, Mhindi anaita hiyo “matembezi ya mauti,” mwajua. Kwa hiyo hivyo ndivyo ulivyo; unaenda ukizunguka. Nami nilijua hilo, lakini ningetokaje?

¹⁵⁵ Na sasa, dhoruba ilikuwa imeshuka moja kwa moja, ikivuma juu ya miti, ukungu ukigeukageuka tu. Nami nikawazia, “Sasa, jambo la busara kufanya...” Ningeliingia mahali fulani, ndani—ndani ya pango mahali fulani na kujificha mpaka dhoruba iishe, kisha nipande mpaka mahali pa juu, ndipo nione mahali nilipokuwa, na kuendelea mbele. Lakini nina mke na mtoto kule juu, wangepanda hata wafe usiku huo. Hawakuwahi kuwa msituni maishani mwao. Hawakujua jinsi ya kujishughulikia wenyewe, na kwa vyovyote vile ingewashtua hata kufa. Vema, nilijua wote wawili wangepanda usiku huo; ilinibidi kuwatafuta. Na ni hisia ya jinsi gani, loo, jamani, mtoto mchanga na mke kufa msituni usiku huo.

¹⁵⁶ Na, lakini nilifikiri nilikuwa bingwa sana nisingeweza kupotea msituni. Kwa hiyo ni—nikazunguka; nikawazia—nikawazia, “Vema sasa, hapa sina budi kupitia njia moja.” Nikawazia, “Nilipokuwa nikipanda mlima, upepo ulikuwa ukinikabili usoni. Nilishuka *hivi*, kwa hiyo hiyo ingelitupa *hivi*.” Nikawazia, “Sasa, tufani inayokuja, ilipitia njia gani?”

¹⁵⁷ Sasa pepo zilikuwa zimebadilika, na kwenye vifuko vya hewa na mizunguko, zitavuma kwa njia yoyote ile, zivume

upande *huu* kwa muda, halafu upande *huu* kwa muda. Na loo, na kulikuwa na mawingu, na ukungu ukining'inia; kuvumwani pande zote mbili za mti chini ya sehemu hiyo ya chini, kwa hivyo hakukuwa na kitu chochote kamwe ningeweza kupata kama alama ya kuniongoza. Gome (chini mle, bila shaka upepo haushuki mle kama vile kwenye tufani ya theluji) pande zote mbili zilikuwa nzito; kwa hiyo hakukuwa na kitu kamwe ambacho ningeweza kupata ili kujiondoa msituni.

¹⁵⁸ Kwa hiyo, nikasema, “Vema...” Ni—nikawa... nikaanza kushikwa na wasiwasi. Na mtu yeyote anajua kinachotokea, halafu unapata homa, ndipo ama unajua au unakufa. Kwa hiyo, nikasema, “Loo, jamani.” nikawazia, “Sina budi kutoka huku; sina budi...” Loo, nikasema... nikaketi kwa dakika moja, nikasema... nikajipiga-piga usoni, nikasema, “Tazama hapa, William Branham, hujapotea. Una shida gani, jamani? Unajua jinsi ya kutoka hapa.” Nilikuwa najidanganya.

¹⁵⁹ Nilikuwa nimepotea, hakika nilikuwa nimepotea. Nikasema, “Mbona, wewe ni bingwa sana msituni huwezi kupotea. Masalale, babu yako angekuwazia nini, kukuona umeketi hapa ukitenda hivi? Mbona, inuka utoke hapa.” Nikaamka na kwenda mbele kidogo, nami ningali nilikuwa nimepotea, hamna lingine. Ndipo nikasema, “Vema, ni lazima nifanye... Lazima nitoke hapa kwa njia fulani.” Kwa hiyo nikasema, “Nitafanya njia ya mkato moja kwa moja *hivi*.” Nami nikasema, “Sitabadilisha hata kidogo. Ninaenda moja kwa moja *hivi*, nami ninajua nitatokea moja kwa moja kwenye Mlima Tufani. Laiti ningaliweza kuona Mlima Tufani, vema, ningejua mahali ule mnara ulipokuwa, ndipo ningeweza kushukia hapo. Sina fununu kama niko mashariki yake, ama magharibi yake, wala mahali nilipo.”

¹⁶⁰ Kwa hivyo ukungu unavuma tu, misitu inapasuka, kwa hivyo nikasema, “Mimi hapa ninaenda, moja kwa moja *hivi*.” Ndipo nikaanza kwenda, kwa vishindo. Kitu kikiniambia, papo hapo sikioni mwangu, kikasema, “Mimi ni Msaada upatikanao wakati wa shida.” Niliendelea kwenda mbele tu. “Mimi ndimi Bwana; mimi ni Msaada utakaonekana tele wakati wa shida.”

¹⁶¹ Nikawazia, “Angalia hapa, na—najua ninatoka, sasa. Kuna kitu kinaniendea kombo. Mnaona?” Nikasema, “Ninasikia sauti. Mimi... Nina—nina shida fulani.” Nikasema, “Angalia hapa, hebu nijinyooshe, jamani, una shida gani? Inakupasa kuendelea mbele. Hujapotea. Unajua mahali ulipo hasa, sasa endelea.” Nami nikawazia, nikatazama *hapa* chini; tayari ilikuwa saa kumi na nusu alasiri. Nikawazia, “Loo, jamani, nilipaswa kuwa kule adhuhuri. Mke ana vipindi vya kupiga mayowe, sasa.” Maana alijua... Mtoto yule, mwituni, hakuwahi kuwa mwituni maishani mwake, mtoto yule mchanga kule juu, hata asingejua jinsi ya kuwasha moto, hajui kitu.

¹⁶² Kwa hiyo, halafu wangenihofia nikiwa huko nje hivyo, wa—

wanaogopa wanyama wa mwituni, na, hapakuwa na kitu cha kuwadhuru, bila shaka, bali wali—waliogopa. Na kwa hivyo nikaendelea tu kusonga mbele, na nikaendelea kusikia kitu Fulani kikisema, “Mimi ni Msaada uliopo kwa wingi wakati wa shida. Ninii. . . Mimi ni Bwana. Mimi ni Msaada uliopo kwa wingi wakati wa shida.”

¹⁶³ Nikasimama na kuwaza, “Sijui kama huyo anaweza kuwa ni Yeye anayezungumza?” Nikasema, “Je, mimi ni mwanamume vya kutosha kukubali ya kwamba nimepotea? Je, mimi ni mwanamume vya kutosha kukubali ya kwamba nimepotea?” Nikavua kofia yangu, na kuiweka chini, nikasema, “Mungu mpendwa, nimepotea. Nimepotea; sijui mahali nilipo. Sijui jinsi ya kutoka hapa.” Nikapiga magoti kwenye kofia yangu, kisha nikaegemeza bunduki yangu kwenye mti.

¹⁶⁴ Nikasema, “Baba, nimepotea kabisa, mimi. . . kwa kuhisi kujitegemea huko ndani yangu, ni—ninastahili kufa. Lakini, Bwana, mrehemu maskini mke wangu na mtoto mchanga huko nje. Watakufa pia. Wanastahili kuishi, nami sistahili. Lakini mimi, Bwana, nimepotea na je, utanisaidia kwa ajili yao?”

¹⁶⁵ Nikasema, “Sijui la kufanya. Endapo huyo ni Wewe unayezungumza, ukisema Wewe ni Msaada utakaonekana tele wakati wa mateso, Wewe kuwa Dira yangu sasa. Unitoe. Hakuna ishara zozote za kimaumbile karibu nami. Lakini nimepotea. Je, utanisaidia?”

¹⁶⁶ Nikasimama, nikapangusa macho yangu, nami nikawazia, “Vema, Mungu, Wewe unielekeze. Mimi hapa ninaenda, sijui nipitie njia gani, lakini nitatembea. Ninaamini nilikuja *hivi*.” Nikasema, “Ninaenda, sasa hayo ni maoni yangu mwenyewe, naenda *hivi*.” Nami nikaweka kofia yangu chini, nikachukua bunduki yangu, nikaanza kwenda *hivi*.

¹⁶⁷ Sasa, kwa kweli kadiri ninavyosimama kwenye jukwaa hili usiku wa leo, Biblia hii, nilihisi Mtu fulani akiweka mkono Wake begani mwangu. Nami nikageuka kuona alikuwa Nani, na wakati nikigeuka tu, ukungu ukatanzuka, nyuma *hivi*. Nami nikauona ule mnara kwenye Mlima Tufani, nyuma *huku*.

¹⁶⁸ Niligeuka *hivi* upesi sana na kujikabili, nikavua kofia yangu, nikatupa chini bunduki yangu, nikainua mikono yangu. Nikasema, “Ee Mungu, loo, jinsi ninavyothamini jambo hili. Bwana, nilikuwa nikiingia Canada moja kwa moja. Ninge kuwa. . . Nisingeweza kutoka humo.” Nikasema, “Bwana hayo yalikuwa maoni yangu mwenyewe.”

Na wakati mwingine, ukichukua maoni yako mwenyewe, utaenda kombo kila wakati. Omba na umwulize Mungu cha kufanya.

¹⁶⁹ Basi nikaangalia kuelekea huko; nikawazia, “Sina budi kuelekeza uso wangu moja kwa moja *hivi*.” Sasa, ukungu ukafunika tena. Ulitanzuka vya kutosha niweze kuona kwamba

ninii . . . Nilijua kama ningeweza kufika kwenye mnara huo ama kuvuka nyaya zile upande ule wa mlima . . .

¹⁷⁰ Nilimsaidia msimamizi kuweka nyaya hizo za simu zilizotelemka hadi kwenye kambi ambapo mke wake alikaa wakati wa kiangazi. Nami nilijua kama ningeweza kuifikia hiyo, ningeukamata waya huo, haijalishi dhoruba ilikuwa mbaya kiasi gani, ningeweza kupata njia ya kwenda kwa familia yangu. Nami . . . nilipokuwa nimesimama pale nikitazama upande *ule*, kitu Fulani kilinijia, kikasema, “Naam, ulikuwa umepotea tena vibaya kuliko hivi. Lakini elekeza tu macho yako Kalvari.”

¹⁷¹ Nikaanza kwenda *hivyo*, nikitembea, nikitembea. Nisingeweza kukwepa; nisingeweza kuzunguka; ingenitupa nje ya mwelekeo wa—wangu. Nilikuwa karibu, angalau maili tano kutoka kwake nalo giza linaingia papo hapo. Nami nikapitia vichakani, nao kulungu wakaruka mbele yangu. Ningeanguka na kuikwaruza miguu yangu kabisa. Giza nzito, nami nilikuwa nikijivuta basi nikijaribu kupanda miamba hii na kadhalika, nikijaribu kuweka mwendo wangu vizuri tu nilivyoweza.

¹⁷² Nikawazia, “Niko juu sasa, inaonekana.” Sasa, sikuweza kuona waya huo, kwa hiyo nikainua tu mikono yangu juu *hivi*. Niliweka bunduki yangu juu ya bega langu katika kombeo, nikainua mikono yangu, na kuendelea tu kutembea. Nikasema, “Nimeinua mikono yangu, Bwana. Acha niushike waya huo nitakapopita juu yake.” Theluji ikinipiga usoni, na kichaka, nikaendelea kutembea; na muda si muda mwajua, kitu fulani kikaugusa mkono wangu. Nikakihisi; kilikuwa ni waya ule. Loo, jamani, hamjui ilikuwa ni hisia ya jinsi gani. Nilijua kama ningeufuata waya huo, nisiuondoe mkono wangu kwake, niufuate waya huo moja kwa moja chini ya kilima kile kama maili mbili na nusu au tatu, ningekuwa papo hapo na mke wangu na mtoto mchanga chini ya hicho kilima.

¹⁷³ Hilo hapo likanijia: Naam, kila mtu aliyetenganishwa na Mungu, akakatiliwa katika ulimwengu huu, pasipo kujua anakoenda, amebebwa kila mahali. Lakini kama utaangalia Kalvari, umwinulie Mungu mikono yako, na umkubali Kristo kama Mwokozi wako mpaka kitu fulani kiupige mkono wako, hiyo ndiyo njia ya kwenda Nyumbani. Fuata uongozi wa Roho Mtakatifu basi. Shikilia mkono wako katika mkono Wake usiobadilika; utakuongoza moja kwa moja hadi kwa Mpenzi wako, Bwana Yesu. Unaamini?

Twaweza kuinamisha vichwa vyetu kwa muda kidogo tu, tuombe?

¹⁷⁴ Baba yetu wa Mbinguni, ninawazia juu ya ule wimbo wa kale, uliosema, “Wakati mmoja nilipotea, lakini sasa nimepatikana, nilikuwa kipofu lakini sasa naona.” Nami ninawazia juu ya ile dhoruba yenye kupofusha usiku ule, moyo

wangu ukirukaruka, homa ikitanda mwilini mwangu, nikiogopa hata kufa, nikijua ya kwamba ningeangamia usiku huo, na vivyo hivyo mke wangu na mtoto mchanga.

¹⁷⁵ Mungu, kunaweza kuwa na wanaume na wanawake walioketi hapa ndani usiku wa leo, ambao pia, wako katika ulimwengu wa kiroho, katika utabiri uo huo. Familia yao itaangamia ikiwa baba hatakuja, au mama, mmojawapo, haraka. Watoto watapeperushwa hapa ulimwenguni. Wajalie usiku huu, waangalie kupitia umande huu wa ukungu unaoning'inia juu ya nchi na waione Kalvari, wainue mikono yao kwa Bwana Yesu, na kugusa Njia ya Uzima inayoelekeza Nyumbani.

Tujalie, Bwana, usiku wetu wa mwisho katika mfululizo huu wa ibada, bariki kila mwanamume ama mwanamke mpotovu, aliyepotea.

¹⁷⁶ Labda waliamini katika mkono wa nyama. Labda wametumainia kanuni za imani za kanisa fulani, lakini kamwe hawakugusa huo Waya. Kamwe hawakupata lile hakikisho lililobarikiwa moyoni mwao, ya kwamba *huu* ndio Waya unaoelekeza kwenye furaha, uhuru, na kwa Bwana Yesu, ule Waya utokao Kalvari hadi Utukufuni.

¹⁷⁷ Jalia kila mtu mweusi, anayeyumbayumba, aliyetengwa katika hili jengo usiku aunyoshe mkono wake, Baba, apapase kwa muda mfupi tu. Watagusa Kitu kitakachotia nanga imani moyoni mwao kitakachowaelekeza Utukufuni.

¹⁷⁸ Huku tumeinamisha vichwa vyetu, kila mtu akiomba. Nikirudi mwaka mmoja kuanzia leo, wengi wenu hapa hamtakuwa hapa. Watu elfu mbili, nadhani, hapa ndani usiku wa leo; mtu fulani ataponyoka nje. Umekuwa ukiyumba gizani? Umekuwa ukija kwenye mikutano, unaangalia, na unaona ishara za Bwana Yesu aliyefufuka; Unasikia Neno; Yeye amekuwa akizungumza nawe kule nyuma, nawe unayumbayumba gizani. Je, utamwinulia mkono wako usiku wa leo, na kusema, "Bwana Yesu, na—nataka kugusa Kambaokozi, sasa, ninainua mikono yangu, mimi. . ."? Mungu akubariki, ndugu. Mungu akubariki, dada. Mungu akubariki, naam, wewe. Hiyo ni kweli, kila mahali. Mungu akubariki, mama, pamoja na. . . Mungu akubariki, kijana. Mungu akubariki, mvulana mdogo. Huko nyuma kabisa, yeyote anayesimama kule nyuma, angesema. . . ?

¹⁷⁹ Inua mkono wako, si kwangu, kwa Mungu. Mungu akubariki, ndugu Mhispaniola. Mungu akubariki, ewe msichana. Mungu akubariki, huyo mama mzungu unayeketi hapo. Juu kwenye roshani, upande wangu wa kushoto, naam wote, angalieni huko juu kwenye ile mikono pale. Jisikieni tu hapo kwa dakika moja, msemi, "Mungu unirehemu mimi, mwenye dhambi."

¹⁸⁰ Mungu akubariki, mama Mhispaniola hapa chini. Roshani upande wa kulia, inueni mikono yenu, na kusema, "Naam,

ninamwamini sasa hivi; ninatangatanga katika giza la kila namna. Kwa kweli hata sikujua; nimeenda kanisani. Loo, naam, nimeweka jina langu kwenye kitabu. Lakini kwa kweli kuwa na tumaini hilo nililo nalo, mkono wangu sasa hivi, kweli sijawahi kuwa na uhakika huo. Lakini sasa, ninakuja kwa uthabiti juu ya msingi wa Damu iliyomwagika ya Yesu na nguvu Zake za ufufuo. Na huyo Roho aliyefufuka anazungumza na moyo wangu, nami ninainua mikono yangu sasa hivi, kusema, ‘Mungu, hapa niliinua mkono wangu kwa ajili ya Kambaokozi.’”

¹⁸¹ Dazeni nyingi wameinua mikono yao. Je, mtu mwingine utainua mkono wako sasa, ambaye hukuinua mkono wako muda mfupi uliopita, popote? Mungu akubariki hapa, ndugu. Mungu akubariki. Mungu akubariki hapa, dada. Mungu akubariki huko nyuma, ndugu. Mungu akubariki, dada; naona mkono wako. Mtu mwingine? Mungu akubariki, ndugu, huko nyuma; naona mkono wako. Mtu mwingine? Mungu akubariki, wewe, wewe hapa, maskini huyo msichana aliyeinua mikono yote miwili. Mtu mwingine? Huyu mtu anayeketi hapa, Mungu akubariki, bwana. Hiyo ni njia nzuri ya kuponywa, ni kumkubali tu Bwana namna hiyo. Mtu mwingine? Mvulana mdogo hapa aliyeinua mikono yote miwili, Mungu akubariki, mpenzi. Mtu mwingine? Mama mmoja hapa, mzee, ameinua mkono wake juu, naam: “Nimepoteza miaka mingi, lakini naja Nyumbani sasa.”

¹⁸² Mungu akubariki kijana mwanamume. Mungu akubariki hapa, ndugu. Mtu mwingine? Kumbuka, unapoinua mkono wako, na kumaanisha kutoka moyoni mwako, Mungu anawajibika kufanya hivyo papo hapo. Mungu ambariki huyu dada mweusi aliyeketi hapa. Ndugu aliye hapa ameinua mkono wake juu, amevaa sweta ndogo ya kahawia, Mungu akubariki. Mungu ambariki huyu mama anayeketi hapa; hiyo ni kweli, dada.

¹⁸³ Yesu alisema, “Yeye ayasikiaye Maneno Yangu, na kumwamini Yeye aliyenipeleka, yuna Uzima wa milele,” sasa hivi. Mungu akubariki, ndugu kule nyuma, mikono yote miwili juu, sasa hivi unampokea Yesu. Mungu akubariki, bwana. Mungu akubariki, mama. Mungu akubariki, bwana. Mungu akubariki, bwana, kijana mwanamume hapo, ndani tu ya . . .

¹⁸⁴ Yesu alisema nini? “Unao, sasa hivi, Uzima wa milele. Yeye ayasikiaye Maneno Yangu,” nimejitahidi niwezavyo kabisa kuwaletea ninyi hayo, “sasa anamwamini Yeye aliyenipeleka, yuna Uzima wa milele wala hataingia hukumuni.”

¹⁸⁵ Mungu akubariki huko juu, dada, unayesimama kando ya nguzo, msichana mdogo Mhispaniola. “Yuna Uzima wa Milele, hataangamia kamwe, hataangamia kamwe...” limaanishe kutoka moyoni mwako. Mungu akubariki, mama; mwanamke mkongwe; mtu anapaswa kumsaidia kuinua mkono wake juu; nawe unamjia Bwana Yesu.

¹⁸⁶ Wasema, “Ndugu Branham, hiyo...hiyo ina maana gani?” Hiyo ina maana kwamba umepita kutoka mautini kuingia Uzimani, papo hapo. Mungu atayashughulikia hayo mengine, kuhusu kukupa Roho Mtakatifu. Wakati mmoja tu limaanishe tu moyoni mwako; mwache Kristo aje moyoni mwako, ndipo utakua katika neema ya Mungu. Mungu atakufunulia tu jambo hilo. Kwanza anza vizuri. Shuka chini, “Imani, kwa imani mmeokolewa, kwa neema, si kwa matendo, mtu awaye yote asiye akajisifu.” Hakuna unachoweza kufanya, kuacha kufanya *hivi*, au kuacha kufanya *vile*. Amini tu; Mungu hukuokoa kwa neema.

¹⁸⁷ Mungu akubariki, dada, uliyeinua mkono wako, hapo. Mungu akubariki, bi mdogo huko nyuma. Na wewe, wewe, wewe, loo, jamani, hiyo ni kweli, wapya wakiinua tu mikono yao kila mahali, wakimkubali Bwana Yesu. Jamani, nadhani tuko karibu sitini ama sabini sasa. Mtu mwingine inua mkono wako, ambaye hajainua mkono wake, na kusema, “Nikumbuke, Mungu.”

¹⁸⁸ Mungu akubariki, maskini jamaa mdogo, msichana mdogo hapo aliyeinua lesu yake. Mahali pengine popote kabla hatujaingia katika maombi? Mungu akubariki, ninamwona yule mtu kule nyuma, naam, kule nyuma, yule ndugu Mhispaniola, kule nyuma akiinua mkono wa mwingine, naam, ninakuona. Mungu akubariki; Mungu anakuona. Mungu ambariki huyo msichana mdogo hapo akiwa ameinua mkono wake juu, mtoto tu, bali akimjia Bwana. Vema, Mungu akubariki hapa, dada. Loo, hilo ni zuri sana.

¹⁸⁹ Tunangoja tu dakika chache, kumpa Roho Mtakatifu wakati wa kunena tu na moyo. Labda anatembea juu ya kusanyiko, akibisha kila mlango. Ni nani Huyu aliyekwambia uinue mikono yako? Ni nani Huyu aliyesema hivyo? Yesu alisema, “Hakuna mtu awezaye kuja Kwangu, asipovutwa na Baba Yangu. Na wote wanijiao Mimi, Baba Yangu akisha kubisha moyoni mwao, wote wanijiao, wanaoinua mikono yao juu kwenye Kambaokozi, nitawapa Uzima wa Milele, nami nitawafufua katika siku ya mwisho.”

¹⁹⁰ Siku moja wakati uhai unapogugumia kooni mwako, labda katika ajali ya barabarani, labda kwa homa, ugonjwa, au mauti tu yakikujia, utakaposikia maumivu ya baridi yakipanda mkononi mwako, marafiki zako wakilia, utamwona Mkombozi yule mbarikiwa akisimama pale na mikono Yake imenyoshwa kuchukua roho yako ili kuiweka ndani ya mwili mpya; mwanamume mpya, kijana mwanamume ama kijana mwanamke, hatazeeka tena, apate kuishi katika Uwepo Wake milele. Kwa sababu, ulilofanya: uliamini tu na kuinua mkono wako.

¹⁹¹ Mungu akubariki, msichana wa kupendeza sana mwenye nywele za kipilipili, za kimanjano anayeketi hapa, akiwa ameinua maskini mkono wake, macho yake madogo yamejaa

machozi, akitazama huku. Mnasema, “Mungu hazungumzi na mtoto huyo.” Hakika anasema naye. Bado hajaufanya mgumu moyo wake kwa mambo ya ulimwengu. Yeye hana hatia, ni mtoto mchanga tu, takriban miaka sita, saba.

¹⁹² Mungu akubariki, dada hapo, huyo msichana. Sasa, kama kuna mwingine tu, kabla hatujafunga. Mungu awabariki, kuna safu nzima yao, inavyoonekana, wanaotokea kule nyuma. Ninachukia kufunga, nanyi bado mnainua mikono yenu kwa ajili ya wokovu.

¹⁹³ Ni wangapi humu ndani sasa wangependa kumpokea Roho Mtakatifu? Mwaweza kuinua mikono yenu? Kote jengoni, kila mahali, jamani, angalieni tu mikono kila mahali; Mungu awarehemu. Twaweza kuomba sasa? Kila mtu huku mumeinamisha vichwa vyenu, macho yenu yamefumbwa.

¹⁹⁴ Yesu alifufuka katika wafu. Loo, jamani, kuwazia ya kwamba huu ndio usiku tunaoagana sasa. Lakini mumemkubali Kristo. Tutakutana tena mahali ambapo hatutaachana kamwe, kwa sababu tu kwamba umemkubali usiku wa leo, hiyo ndiyo tofauti yake.

¹⁹⁵ Baba wa Mbinguni, huu mkutano mkuu wa Phoenix sasa unakaribia kwisha. Na mwishowe, wenye dhambi wengi, wengi sana walikuinulia Wewe mikono yao, juu ya fundisho la Neno ulilosema, “Yeye ayasikiaye Maneno Yangu na kumwamini Yeye aliyenipeleka, yuna Uzima wa milele, hatapotea wala kuingia hukumuni,” kulaaniwa. Hahukumwi tena mbele za Mungu, bali amemkubali Yesu Kristo na mateso Yake badala yake.

¹⁹⁶ Sasa, Baba, kwa utamu, waongoze kwa unyenyekevu, wanaposhikana mikono wakiegemea kwenye Kambaokozi, wakitembea kuelekea Utukufuni. Si utawabariki sasa? Mwokoe kila mmoja wao, Baba. Katika Ufalme Wako, naomba niwaone na niwape mkono. Na ikiwezekana, naomba uweze kuileta tena ibada ya usiku wa leo kwetu. Wangesema, “Naam, hiyo ilikuwa ndiyo, hapo ndipo... huyo alikuwa ni mimi, nikainua mkono wangu.”

¹⁹⁷ Mungu aseme, “Naam, nilikuona. Niliuvuta moyo wako. Uliinua mkono wako; nilikukubali. Na sasa wewe ni mtoto Wangu mpendwa; njoo kwenye furaha za maisha, ulizowekewa tayari tangu kuwekwa misingi ya ulimwengu. Ingia katika furaha.”

¹⁹⁸ Tunakushukuru, Baba. Wale ambao tayari wamekuja na wanataka kujazwa na Roho Mtakatifu, watengwe kwa ajili ya ibada, wajalie wao pia, Bwana. Hatimaye mwishoni mwa safari, maisha yatakapokwisha, ile Karamu kuu ya Arusi imeandaliwa, pale ile meza yenye urefu wa maelfu ya maili, waliooshwa kwa Damu wa nyakati zote wameketi pale, Mfalme atoke, apanguse machozi machoni mwao, aseme, “Hakuna mateso tena sasa;

hakuna sababu ya kulia sasa; Sote tuko hapa; njoni, ninyi mliobarikiwa na Baba Yangu.”

¹⁹⁹ Hadi wakati huo, Baba, uwadumishe wenye furaha nafsini mwao, uwatakase na uchafu wote na udhalimu. Jalia watembea kila siku huku matanga yao yakielekea Utukufuni, wakiwaleta wengine Kwako. Kwa maana tunaomba katika Jina la Yesu, Mwanao mpendwa, Ambaye sasa amewaita kwenye Uzima wa milele. Amina. [Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.]

²⁰⁰ Amini kwa moyo wako wote, kwa nguvu zako zote. Ondoa tu hisia zote ambazo unawazia tu, au hisia zote za kishirikina, zitupe tu kando. Kisha mtazame Mungu moja kwa moja na useme, “Ninaamini kwa moyo wangu wote, kwa uchaji.” Kisha angalia uone Roho Mtakatifu atafanya nini.

²⁰¹ Sasa, nyote tayari? Sasa, kwa utukufu wa Mungu, na kwa ushuhuda wa ufufuo wa Yesu Kristo, ninachukua kila roho katika hili jengo chini ya mamlaka yangu. Sasa, iweni na kicho; msisogeesogee, tulieni, tafadhali. Sasa, usiku huu wa kufunga, nipeni fadhila hiyo. Katika Jina la Yesu, sivyo? Iweni tu na kicho kabisa, kaeni kimya. Watanitazama. Hawataniruhusu kwa muda mrefu sana mstarini, halafu basi . . . kwa sababu mimi ni dhaifu sana na nimechoka.

²⁰² Na ninawapenda ninyi nyote kwa upendo moto moto sana wa Kikristo. Mungu awabariki. Kama upako ukinigusa, bila shaka sijui wanaponichukua, au kinachotokea. Nami ninatumaini kuwaona tena, mara moja. Hadi wakati huo nitakuwa nikiwaomba. Mungu awabariki.

²⁰³ Vema, mama. Sasa, naomba uje hapa kwa muda mfupi tu, dada. Sasa, tunadhaniwa, nadhani hatufahamiani. Naam. Umeniona, lakini ninamaanisha . . . kutokukujua wewe. Mimi—mimi . . . kama ninakujua, sitambui hilo. Sikutambui. Nasi tumeonana tu namna hiyo, ungekuwa kwenye kusanyiko na kuangalia tena na kuniona.

²⁰⁴ Lakini kujua wewe ni nani, uko wapi, imekuwaje, hilo—hilo haliwezekani, sivyo? Isipokuwa tu ingefunuliwa kwa ufunuo wa kiroho, au ono, ama njia fulani ya kujua. Sina fununu zaidi ya kile kilichokuleta hapa, kuliko ninavyojua, vema, kilichomleta mtu mwingine yeyote. Unaona? Sikujui; lakini Yeye anajua kilichokuleta hapa. Naye anaweza kuniambia kwa nini uko hapa; anionyeshe ni kwa nini uko hapa. Ningeweza kukwambia, kama ni kwa ajili ya uponyaji wa mwili wako basi, vema, Mungu angeninii . . . ungeweza kufanya hivyo kwa imani yako, ukiamini.

²⁰⁵ Naona wewe ni mfanyakazi wa binafsi. Kwa hivyo, lakini ikiwa Yeye—kama Yeye atanijulisha kwa nini uko hapa . . . Sasa, ninazungumza nawe kama vile tu mwanamume kwa mwanamke, kama tu Yesu kwa yule mwanamke kule Samaria.

²⁰⁶ Sasa, kwa wasikilizaji, huyu hapa mwanamke nisiyemjua. Huenda mnamfahamu. Unatoka hapa Phoenix, sivyo? Unatoka

Phoenix? Watu huko nje wanamjua, sivyo? Vema, simjui. Sijawahi kumwona maishani mwangu. Lakini mnajua kama hii ni kweli au la. Nanyi mnajua kama ninajua lolote kumhusu au la. Sina njia; simjui huyu mwanamke, sembuse kujua chochote kumhusu.

²⁰⁷ Sasa, njia pekee hilo lingefanywa, kama lingefanywa katika kanuni za Kimaandiko, sasa ondoeni kutoka ya kale namna fulani ya kanuni za imani mlizojifunza na tuangalie Biblia. Yesu alisema, “Mambo nifanyayo Mimi, ninyi nanyi mtayafanya.” Sasa, alipokutana na mwanamke kama huyu, alianza kuzungumza naye. Na muda si muda mwajua, Yeye alipata mahali hasa ambapo shida yake ilikuwa. Na katika kisa hicho, alikuwa mwanamke ambaye alikuwa na waume watano. Kasema, “Nenda—nenda kamwite mumeo.”

Akasema, “Sina yeyote.”

Kasema, “Una watano.”

²⁰⁸ Akasema, “Naona kuwa Wewe ni Nabii.” Kasema, “Ninajua ajapo Masihi, hiyo itakuwa ndiyo ishara Yake.” Unaona, ishara ya Masihi, kufanya jambo hilo. Watu siku hizi wanasema ni telepathia ya kiakili, ni ibilisi. Si ajabu tuko katika hali tuliyomo. Ni Bwana Yesu aliyefufuka, ishara ya Masihi.

Lakini alisema, “U nani Wewe?”

Akasema, “Mimi Ndiye.”

²⁰⁹ Akakimbilia mjini na kusema, “Njoni, mwone.” Likaanzisha uamsho katika mji huo, kwa sababu tu ya ushuhuda wa mwanamke mmoja, Yeye akimwambia... akimwambia jambo moja. Na kama hiki si kisa kama hicho kabisa, nje ya kujua shida yake, usiku wa leo, sivyo? Kila mtu anatambua hilo?

²¹⁰ Sasa, wewe... yeye ni mwanamke wa Phoenix, alisema. Nanyi nyote mnamjua. Wengi wenu mliinua mikono yenu; mnamfahamu. Sasa, Bwana anaweza kuniambia ana shida gani. Lakini ikiwa yeye—ikiwa yuko hapa kwa ajili ya shida za kinyumbani, matatizo ya kifedha, au uponyaji, mgonjwa, au chochote kile, ama kwa ajili ya nafsi yake, chochote kile, Mungu anaweza kulifunua. Naye atajua kama hiyo ni kweli au la. Ndipo basi ikiwa anajua yaliyokuwapo, hakika Yeye anajua yatakayokuwapo.

²¹¹ Sasa, kila mtu awe na kicho. Sasa, ninapozungumza na mwanamke huyo, ili tu kuishika roho yake. Sasa, kidogo ninakungojea utulie, ukiweza. Msisogeesogee. Kuna kila namna ya roho humu ndani usiku wa leo, mnaona, zinazosogea, ninamaanisha ugonjwa. Nami ninaona, haswa watoto. Watoto, huwafikia watoto kwa urahisi sana. Kwa hivyo msininii—msininii... Mara niliposema hivyo, kifafa kilianza kuvuta. Na hiyo ni kweli. Na hilo ndilo jambo ambalo... Mara tu hawa... Ninyi—ninyi—ninyi...

212 Nawaambia, ili kujua mambo ya kiroho, marafiki, angalieni jinsi maneno yatakavyobadilisha mitazamo ya kiroho na kadhalika. Mnaona? Mara aliponisikia nikisema hivyo, basi kifafa kikaanza kujongea ndani.

213 Sasa, sasa nataka tu kuzungumza nawe kwa dakika moja, kusudi tu niione roho yako ya kibinadamu. Sasa, Mungu akipenda... Wewe ukiwa, wewe ni Mkristo mwaminio. Na kama Mungu ataondoa, ama kuingia ndani na kuniambia kwa nini uko hapa, basi utaamini; utajua, ukiamini inatoka kwa Mungu.

214 Jambo la kwanza, una kitu kibaya kwa kula; kinahusu ugonjwa wa tumbo. Una tatizo la tumbo, ambalo ni ugonjwa tumboni kwa sababu husababisha vitu kuja kinywani mwako na kadhalika. Ni ugonjwa wa tumbo.

215 Kisha una m—mkono ambao ni mbaya. Na huo ni mkono wako wa kushoto. Nao ulipondwa na gari. Hiyo ni kweli. Unaamini sasa? Unaamini sasa? Njoo hapa, dada.

Baba wa Mbinguni, ninaomba ya kwamba utabariki sasa. Mpe shauku ya moyo wake, katika Jina la Yesu Kristo, ninaomba. Amina. Amina.

216 Amini, amini kwa moyo wako wote. Sasa, hatufahamiani kabisa. Sasa, hii hapa picha kamili ya Bwana Yesu kisimani. Yeye alikuwa Myahudi, naye mwanamke huyo alikuwa Msamaria, hali ya kijamii, kama tu ilivyo leo, mimi nikiwa mzungu, wewe mwanamke mweusi. Lakini ni... Yesu aliwajulisha, upesi sana, haikuleta tofauti yoyote kwa Mungu. Sisi sote tumetokana na mtu mmoja. Sisi sote ni watoto wa Mungu.

217 Lakini kama ni Myahudi, Mmataifa, mweupe, mweusi, manjano, kahawia, haijalishi. Mungu, kwa Damu moja, kupitia Mwanawe, Yesu Kristo, ametununua, kila mmoja. Na katika hilo, tunakuwa ndugu na dada. Sasa, mimi nikiwa mgeni kwako, unaamini ya kwamba Mungu atakufanyia jambo fulani, kama Yeye...?

218 Sasa, unajua sikujui, sivyo, mama? Si—si... Hatufahamiani. Lakini u—unaugua u—ugonjwa wa fadhaa. Una wasiwasi, umevurugikiwa. Una mambo mengi sana moyoni mwako, huzuni. Umevurugikiwa kabisa kuhusu jambo fulani. Ninaona giza likiingia, linazidi kuwa giza. Inaonekana kuna mtu amesimama kule nyuma, lakini ni mwanamume. Naye anayumbayumba; anakuja nyumbani. Ni mume wako; yeye ni mlevi. Nawe uko hapa... Mrehemu, Mungu. Vema. Hiyo ni kweli, dada. Njoo karibu.

Baba, ninaomba ya kwamba utamtimia haja yake, katika Jina la Yesu Kristo. Amina. Mungu akubariki.

219 U hali gani, dada? Nataka mwe na kicho, kila mahali. Tafadhali msisogee. Sasa, mama, tunafahamiana?

Hatufahamiani? Hatufahamiani kabisa? Naam, Yesu Kristo Mwana wa Mungu alikufa kuokoa . . .

²²⁰ Una kasoro ubavuni mwako, sivyo, dada, unayeketi hapo, papo hapo mbele? Una shida ubavuni mwako. Jambo la kigeni sana lilitokea wakati mama huyo dakika chache zilizopita alipoambiwa jambo fulani kuhusu mpendwa wake, kwa sababu unamwomba mpendwa pia: Huyo ni baba ambaye hajaokoka. Ninamwona amesimama, nawe unamwomba. Hiyo ni kweli, sivyo? Mungu akubariki, ewe msichana.

Sasa, hapo wewe . . . Hao wawili, wote wawili wameketi hapo hapo mwishoni, wakiagua kifafa. Hiyo ni kweli.

Ewe pepo, katika Jina la Yesu Kristo, waache, toka ndani yao.

²²¹ Unaamini sasa, mama, kwa moyo wako wote? Unaamini ya kwamba Yesu Kristo Mwana wa Mungu yuko hapa kukuponya? Naamini unaamini. Wewe, unatambua ya kwamba sasa hivi, uko katika Uwepo wa Kitu fulani, sivyo, dada? Ni Uwepo Wake. Je, si ni hisia ya ajabu kusimama katika Uwepo huu? Sasa, kama hiyo ni kweli, ili wasikilizaji waone, inua mkono wako; faraja hiyo ya ajabu ya upendo, kama kumimina.

²²² U—unaagua ugonjwa wa mapafu yako, tatizo la mapafu. Inaonekana kana kwamba ulikuwa na kitu . . . Je, ulitolewa ubavu ama kitu fulani, aina fulani ya shida ya ubavu? Ni chini ya ninii yako . . . Mbavu zilisogezwa, naam. Niliwaona wakichukua au kufanya kitu kwenye mbavu.

²²³ Nawe una . . . una m—mpindiko wa uti wa mgongo. Pia una tatizo la tumbo, maana limesukumwa, nao walisema tumbo limesukumwa vibaya. Kisha unaumwa na mgongo wako. Hiyo ni kweli. Unaamini Yesu yuko hapa kukuponya? Basi kama huyo ni Yeye anayezungumza, basi sio mimi. Njoo, hebu niweke mikono yangu juu yako.

Mungu, katika Jina la Bwana Yesu Kristo, mponye dada yetu na yote anayomba, katika Jina la Yesu. Amina.

Amini; usiwe na shaka.

²²⁴ Sasa, dada, unayeketi hapo ukiwa na shida ya ini, unayeketi papo hapo, ulikuwa unaomba wakati huo. Ulisema, “Mungu, jalia aseme nami nami nitakuamini Wewe.” Si hivyo ndivyo ulivyosema hasa? Inua mkono wako ikiwa hiyo ni kweli kabisa. Sasa, simama kwa miguu yako. Shida ya ini imekuacha, dada.

²²⁵ U hali gani, bwana. Unaamini? Hatufahamiani, ndugu. Lakini Yesu Kristo anatumia sote wawili. Ikiwa Mungu ataniambia ni kwa nini hasa uko hapa, je, utakubali ulichokujia, kupitia kwa Yesu? Sivyo? Kuna kivuli cha mauti kinachoning’inia juu yako. Na hicho ni tatizo tumboni mwako. Na hiyo ni kansa tumboni. Unaamini sasa, ya kwamba Yesu

Kristo atakuponya? Unaupokea sasa hivi juu ya msingi wa Damu Yake iliyomwagika? Basi nenda ukale.

Katika Jina la Yesu Kristo, ibilisi na amwache ndugu yangu. Amina.

²²⁶ Amini; usiwe na shaka. Yesu alisema, “Kama unaweza kuamini...” Ndivyo hivyo, jamaa mdogo. Amina. Mwanamke yule wa Kihindi aliyeketi pale mwishoni alikuwa ameinamisha kichwa chake akiomba wakati uo huo, ana kichano nyweleni mwake. Malaika wa Bwana, hiyo Nuru, inaning’inia juu ya mwanamke huyo. Anasumbuliwa na mafua yaletwayo na vumbi. Hiyo ni kweli, mwanamke wa Kihindi. Yesu Kristo anakuponya.

²²⁷ Aisee, rafiki yako anayeketi karibu nawe, huyo mwanamke mwingine wa Kihindi hapo, anasumbuliwa na kichwa. Weka mkono wako juu yake pia, ili naye pia aponywe. Inua mkono wako hapo, mama, na upokee uponyaji wako kupitia Yesu Kristo Mwana wa Mungu. Amina. Huo hapo unaondoka: amepona. Mchirizi mzito wa giza unaondoka, ukitoka nje; Kitu cheupe kikiusukuma. Umekwisha. Amini.

²²⁸ Huyu ndiye mgonjwa? Unaniamini, mama, kama mtumishi wa Mungu, kwa moyo wako wote? Sikujui, sijawahi kukuona. Lakini maisha yako, usingeweza kujificha sasa, kwa maana nimewasiliana na roho yako, kupitia Yesu Kristo. Uko hapa kwa jambo linalostahili. Wewe ni mwanamke ambaye amekuwa tasa na unataka watoto. Unataka nikuwekee mikono yangu, ili upate mtoto.

Baba wa Mbinguni, mpe mwanamke huyu shauku ya moyo wake. Ninambariki, kama mtumishi Wako, katika Jina la Mwanao, Bwana Yesu. Amina.

²²⁹ Amini. Usiwe na shaka. Unataka kuondokana na yabisi kavu hiyo, unayeketi hapo nyuma? Simama; imani yako imekuponya, dada. Hiyo ni kweli, simama, onyesha mikono yako hewani, acha watu waone ya kwamba umeponywa. Kabisa, uko huru nayo sasa. Amina. Imani yako inakufanya mzima. Amina. Mwamini Mungu; usiwe na shaka.

²³⁰ Njoo hapa, mama. Unaamini? Hatufahamiani. Hatujuani, nadhani, lakini Yesu Kristo anatumia sote wawili. Roho zinaomba usaidizi. Mimi...Hebu kidogo, mama. Sisi tukiwa hatufahamiani, wala hata hatujaonana, kama mimi, kama Roho Mtakatifu, hasa, kupitia kwangu, angekwambia shida yako ni ipi, ungeamini? Nawe ungeamini kuwa inatoka kwa Mungu?

²³¹ Je, kusanyiko litaamini kuwa inatoka kwa Mungu? Sasa, bila shaka kadiri ningeweza kuongea nawe, ndivyo Yeye angesema mengi, lakini ndivyo amesema. Ninaona kitu fulani kimezungushiwa mkononi mwako. Ni shinikizo kuu la damu, ulilo nalo. Na pia una roho inayokaba. Ni tezi kwenye koo yako, inayosonga, tezi ya ndani. Hiyo ni kweli. Wewe hutoki humu nchini. Umetoka upande wa mashariki. Umetoka Grandview,

Tennessee. Hiyo ni kweli. Hilo lilikushtua? Jina lako ni Bi Lily Edwards, pia. Hiyo ni kweli. Sasa nenda nyumbani ukapone katika Jina la Bwana Yesu Kristo. Amini.

²³² U hali gani? Jambo la kwanza kukwambia, rafiki yangu, ni ma—maisha yako na Mungu. Wewe si... hupendezewi na mwenendo wako. Unataka kutembea karibu zaidi kidogo na Bwana. Hiyo ni kweli. Naona unamsihi katika maombi. Kisha naona una kivimbe. Na hicho kivimbe kinakua. Nacho kivimbe hicho kiko tumboni. Hiyo si ni kweli?

²³³ Je, unataka kutembea karibu zaidi na Mungu? Unataka kuponywa? Basi amini ya kwamba Yule anayeongea nawe (si ndugu yako), ni Bwana Yesu Kristo, apate kukupa hayo. Unaamini? Basi katika Jina la Yesu Kristo, Mwana wa Mungu, pokea kile unachoomba. Amina.

²³⁴ Uko karibu na Ufalme, dada. Mama... (Huyu ndiye mwanamke huyo, huyu ndiye mgonjwa?) Hatufahamiani, nadhani. Sikujui, lakini Mungu anakujua. Wewe ni mwaminio. Hujasimama hapa kwa ajili yako mwenyewe; unasimama kwa niaba ya rafiki. Nawe umepokea namna fulani ya ujumbe kutoka kwa rafiki huyo. Nao wanaenda kufanyiwa upasuaji asubuhi kwa ajili ya kansa. Na hiyo ni karibu na ziwa kubwa au ninii... iko karibu na Chicago, Illinois. Hiyo ni kweli.

Mungu, katika Jina la Bwana Yesu, jalia uponyaji wa chochote anachoomba, kupitia Jina la Yesu.

²³⁵ Bwana Yesu anaweza kuponya ugonjwa wa moyo sawa na vile anavyoweza kuponya chochote. Unaamini hilo? Unaamini utaupokea sasa? Katika Jina la Yesu, nenda ukaupokee. Amina.

²³⁶ Njoo, mama. Unaamini kwa moyo wako wote? (Sina budi kuharakisha tu kidogo; ninii tu, hapana, nishikilieni tu.) Angalia tena huku kwa dakika moja tu. Unaamini? Unataka kwenda kula chakula chako cha jioni? Tatizo hilo la tumbo limekuwa likikusumbua, linavurugika kabisa, mkakamao, uchungu, unakupinda, tatizo la wanawake. Nenda zako, Yesu Kristo akuponya.

²³⁷ Unaamini? Unaamini Mungu atakuponya ugonjwa huu wa anemia? Unaamini unaweza kwenda nyumbani, ukaponywe ugonjwa huu wa anemia? Mungu akubariki. Nenda, ukapokee unachoomba, katika Jina la Yesu.

²³⁸ Vema, njoo mama. Naona ukichechemea unapokuja, magoti. Hapana sivyo, hujavunjika nyonga; ni ugonjwa wa yabisi kavu unaokusumbua. Unaamini wewe... Yesu Kristo atakuponya? Nenda, na ukapone, katika Jina la Yesu.

²³⁹ Hivi utakuja, mama? Unaamini? Unataka kuondokana na tatizo hilo la mgongo na figo? Unaamini Yesu anakuponya? Basi nenda zako, na Yesu Kristo akuponye na kukupa afya kabisa. Amina.

Yabisi kavu yako iliponywa ulipokuwa umeketi pale *chini*, bwana, usiku wa leo. Hunayo tena.

²⁴⁰ Vema, ulipokuwa umeketi pale nje ukinitazama usiku wa leo, papo hapo *chini*, kuna kitu kizuri sana kilichopitia tumboni mwako; kidonda kiliondoka wakati huo. Umepona.

Njoo. U hali gani? Tatizo la moyo limekwisha, ndugu. Nenda zako, ukishangilia na kumsifu Mungu. Amini kwa moyo wako wote.

Macho na tumbo, lakini Yesu Kristo anakuponya.

Amini. Hebu kidogo.

Usiogope; ugonjwa wako wa figo na kila kitu kimekuondokea, mama. Nenda zako, ukiamini.

Ugonjwa wa tumbo, chochote kile, Mungu anaweza kuuponya wote, sivyo? Akupe afya, akuponye kikamilifu.

Katika Jina la Bwana Yesu Kristo, ninaomba dua kwa ajili ya ndugu yangu. Amina.

Sana . . . Angalia, iko kila mahali. Angalieni, inapiga tu kila mahali.

²⁴¹ Una ugonjwa wa moyo, mama. Kila mtu aliye na ugonjwa wa moyo, simama kwa miguu yako kwa dakika moja. Mnaona nilichowaambia? Utatambuaje? Inakuja tu kila mahali. Simama hapa kwa dakika moja tu. Amini kwa moyo wako wote sasa. Simama hapa na . . .

Endeleeni kusimama kwa dakika moja.

²⁴² Angalia hapa, mama; una TB. Kila mtu aliye na TB, simama kwa miguu yako kwa dakika moja. Simameni upesi sana, wagonjwa wa TB. Ku—kuwa mwaminifu; amini kwa moyo wako wote. Mapafu, mapafu, inaendelea kusonga. Hiyo ni sawa, bwana. Wewe simama kwa vyovyote vile. Huna TB, lakini una nimonia kwenye mapafu yako. Hiyo ni kweli, unayesimama papo hapo. Hiyo ni kweli, wewe. Simama kimya.

²⁴³ Mtu huyu aliyelala papa hapa ana nimonia mapafuni mwake, kwenye machela hii. Simama, bwana, Yesu Kristo akuponya. Nyie wengine simameni kwa dakika moja. Simameni.

Ee Mungu, katika Jina la Yesu Kristo, Mwana wa Mungu, ninawaleta Kwako watu hawa wagonjwa na wanaoteseka.

Ninamkemea kila ibilisi ambaye amewafunga watu, TB, kila kitu, vilema wote hawa, wagonjwa, wanaoteseka.

Mungu, katika Jina la Yesu, utoe.

Waache, toka na uwaache waaminio hawa wote.

Simameni kwa miguu yenu kila mahali, mkaponywe. 

55-0302 Bwana Yesu Aliyefufuka
Shriner Temple
Phoenix, Arizona Marekani

SWAHILI

©2022 VGR, ALL RIGHTS RESERVED

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. Box 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org

Ilani ya haki ya kunakili

Haki zote zimehifadhiwa. Kitabu hiki kinaweza kuchapishwa kwa matbaa ya nyumbani kwa matumizi ya kibinafsi ama kusambaza, bila malipo, kama chombo cha kuitangazia Injili ya Yesu Kristo. Kitabu hiki hakiwezi kikauzwa, kunakiliwa kwa wingi, kuwekwa kwenye mtandao, kuhifadhiwa kikatolewe tena, kufasiriwa katika lugha zingine ama kutumiwa kuomba fedha bila idhini halisi iliyoandikwa moja kwa moja kutoka Voice Of God Recordings®.

Kwa habari zaidi ama kwa vifaa zaidi, tafadhali wasiliana na:

VOICE OF GOD RECORDINGS

P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.

www.branham.org